# Nipashe

Jumamosi Januari 27, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581568

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper


**WAWILI** wafariki ziara ya Naibu Waziri Mkuu

UKURASA 3

**ANUSURIKA** kuuawa madai ya kuharibu mashine ya kamari



UKURASA 4

**GHANA** kufungua kiwanda cha kuunganisha magari Tanzania

UKURASA 4



**MO SALAH: NITAPAMBANA KUREJEA AFCON**

UKURASA 22

UHABA SUKARI

# Wanne mbaroni kuuza bei ya juu

**MAKALI** ya bei yatikisa Zanzibar...*Endelea ukurasa wa 2*



Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji

## Mshtuko kujiuzulu kwa Waziri Utalii

UKURASA 3



Simai Mohamed Said

## Makonda sasa atwishwa zigo kuhusu mikopo kausha damu

UKURASA 5

**MICHEZO** SIMBA, YANGA, AZAM ZAGEUKIA FA CUP UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Makatibu Wakuu wa Vyama Sita Marafiki vya Ukombozi Kusini mwa Afrika, wakionyesha nakala ya Katiba ya Usimamizi na Uendeshaji wa Shule ya Uongozi ya Mwalimu Julius Nyerere (MJNLS), baada ya kutia saini, eneo la Kwa Mfipa, Kibaha, mkoani Pwani, jana. Kutoka kushoto ni Katibu Mkuu wa Chama cha ZANU- PF (Zimbabwe)Komredi Obert Moses Mpofu, Katibu Mkuu wa Chama cha SWAPO (Namibia), Komredi Sophia Shaningwa, Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa MPLA (Angola), Komredi Manuel Domingos Augusto, Katibu Mkuu wa CCM, Komredi Dk. Emmanuel John Nchimbi, Mkuu wa Shule ya MJNLS, Prof. Marcelina Chijoriga, Katibu Mkuu wa ANC (Afrika Kusini), Komredi Fikile Mbalula na Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Chama cha FRELIMO (Msumbiji), Komredi Francisco Mucanheia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanne mbaroni kuuza sukari bei juu

**Na Waandishi Wetu**

Wafanyabiashara wanne wa maduka ya jumla katika Manispaa ya Singida, wamekamatwa kwa madai ya kuuza sukari kwa bei ya juu kinyume cha bei elekezi iliyotolewa na Bodi ya Sukari Tanzania.

Wafanyabishara hao ambao majina yanahifadhiwa kwa sababu uchunguzi bado unaendelea, walikamatwa juzi baada ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Singida ikiongozwa na Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Naima Chondo, ilipofanya ukaguzi kwenye maduka na stoo za wafanyabiashara mjini hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuongoza oparesheni hiyo, Chondo alisema kulingana na mwongozo wa bei ya sukari uliotolewa hivi karibuni na serikali, wafanyabiashara wa maduka ya jumla wanapaswa kuuza sukari kwa kilo kuanzia Sh. 2,650 hadi 2,800 wakati wenye maduka ya rejareja wanapaswa kuuza kwa Sh. 2,800 hadi 3,000 kwa kilo.

Chondo alisema baadhi ya wafanyabishara katika Manispaa ya Singida wamebainika kuuza kwa Sh.3,700 hadi 4,000 kwa kilo katika maduka ya rejareja wakati wale wa maduka ya jumla wamepandisha bei hadi Sh. 185,000 kwa mfuko wa kilo 50.

Alisema kutokana na mabadiliko hayo ya bei, serikali wilayani Singida imefanya msako wa wafanyabishara walipandisha bei za baadhi ya wafanyabishara na kuwakamata wanne waliokiuka mwongozo wa bei zilizotolewa na serikali.

"Tunawaomba sana wafanyabiashara wa Singida na hususani wilaya ya Singida, kufuata taratibu, kanuni na sheria. Hii bidhaa pamoja na bidhaa zingine zote zina bei elekezi, hivyo tuuze kwa bei elekezi na waelewe pia kuficha bidhaa ni kosa la uhujumu uchumi," alisema.

Wakala wa usambazaji wa sukari mkoani Singida , Nagji, alisema kulingana na bei elekezi ya serikali, anauza sukari kwa Sh.140,000 kwa mfuko wa kilo 50 kwa bei ya jumla na kwamba tayari magari mawili yaliyobeba sukari yamewasili, hivyo kushauri wafanyabiashara wengine kutoongeza bei.

Mkuu wa Idara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji Manispaa ya Singida, Erick Sinkwembe, alisema hakuna sababu kwa wafanyabiashara kuongeza bei kwa kuwa wakala wa usambazaji amepokea mifuko 620 sawa na tani 32 juzi na kwamba mifuko mingine 660 inatarajiwa kupokewa hivi karibuni katika Manispaa ya Singida na wilaya za jirani.

Sinkwembe aliwataka wafanyabiashara kuzingatia bei elekezi ili kuondoa adha kwa watumiaji.

Aidha, aliwatoa hofu wananchi na wafanyabiashara kwa kuwahakikishia uwapo wa sukari na kusisitiza kutopandisha bei wala kuficha bidhaa hiyo kwa kuwa sukari iliyopokewa inatosheleza.

**DC MKALAMA**

Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, Moses Machali, aliwataka wafanyabiashara wilayani humo kuuza sukari kwa mujibu wa bei elekezi ya serikali na kuwaonya wenye tabia ya kuficha bidhaa hiyo kwamba atayebainika kufanya hivyo atachukuliwa hatua za kisheria

Alisema hayo juzi baada ya kumaliza ukaguzi na kuwabaini wafanyabiashara wanaouza sukari bei juu tofauti na maelekezo yaliyotolewa na serikali kupitia Bodi ya Sukari Tanzania.

"Bei ya rejareja ya sukari katika mkoa wa Singida kwa mujibu wa Bodi ya Sukari haipaswi kuzidi Sh. 3,000. Tutakayemkuta anauza sukari zaidi ya Sh. 3,000 tutamkamata. Mnasababisha maisha ya wananchi kuwa magumu, hivyo hatuwezi kuruhusu hilo," alisema.

Aidha, Machali aliwakumbusha wafanyabiashara hao kuwa na stakabadhi za malipo pindi wanaponunua sukari kutoka kwa wasambazaji wakubwa ili kubaini kwa nini wanauza bei kubwa tofauti na maelekezo yaliyotolewa na serikali.

**MAKALI BEI ZANZIBAR**

Kutoka Zanzibar, imeelezwa kuwa makali ya bei yameanza 'kung'ata' Zanzibar huku ikidaiwa ikiwa inasafirishwa kwa wingi kwenda Tanzania Bara baada ya wasafiri wengi wanaotoka huko kwenda Bara wakiwa wamebeba wastani wa kilo tano kila mmoja.

Kwa mujibu wa uchunguzi, kilo moja ya sukari Zanzibar kwa sasa inauzwa Sh. 3,200 kwa mfuko wa kilo moja huku kilo tano ikiuzwa kwa Sh. 17,000. Awali kilo moja ilikuwa ikiuzwa kati ya Sh. 2,500 na 2,700 wakati mfuko wa kilo tano ulikuwa Sh. 12,000 hadi 14,000.

Ofisa Biashara kutoka Wizara ya Biashara na Masoko, Said Abdallah Khamis, alisema Zanzibar ina kiwanda kimoja cha uzalishaji bidhaa hiyo ambacho hakitoshelezi kwa mahitaji, hivyo kuagiza Brazil na India.

Alisema kwa sasa kuna upungufu wa bidhaa hiyo kutokana na uzalishaji mdogo na changamoto mbalimbali katika mataifa hayo. Alisema India walikuwa na uchaguzi na Brazil kuna ushindani mkubwa wa kibiashara na kwamba China inaagiza sukari kutoka huko.

***Imeandikwa na Thobias Mwanakatwe (SINGIDA) na Rahma Suleiman (ZANZIBAR).**

# AMREF yabuni mpango kunusuru walioacha ARV

**Na Ibrahim Joseph ,** DODOMA

SHIRIKA la AMREF Tanzania limeanzisha mkakati wa kunusuru watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI (WAVIU) ambao wamekuwa wakiacha matumizi ya dawa za kufubaza makali virusi (ARV) kwa sababu ya unyanyapaa.

Mkurugenzi wa Mradi wa Afya Thabiti wa AMREF, Dk. Edwin Kilimba, aliyasema hayo jana kwenye mkutano wa mazungumzo kati ya shirika hilo, Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Alisema AMREF Tanzania kupitia mradi wa Afya Thabiti wameanzisha mpango huo baada ya kubaini idadi kubwa ya WAVIU wanaacha kutumia dawa kwa sababu ya unyanyapaa.

Kutokana na hali hiyo, wameanza kutoa elimu kwa wahusika pamoja na kuwa na mpango wa kuwaruhusu wahusika kuchukua dawa ambazo watatumia kwa muda wa miezi mitatu au sita bila kuhudhuria kila siku kliniki .

"Tumebaini wanakimbia matumizi ya dawa hizo kwa sababu ya unyanyapaa kutoka kwa watu wengine hasa ndugu wa karibu na marafiki. Utaratibu huu utawaruhusu wale ambao hawasumbuliwi na magonjwa nyemelezi kuchukua dawa za kutumia kwa muda mrefu," alisema.

Pia alisema kupitia mradi huo watatoa elimu ya afya, kuboresha huduma za tiba, kuratibu na kutengeneza sera na miongozo mbalimbali ya kiafya.

Meneja wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI, Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini (NASHCOP) kutoka Wizara ya Afya, Dk. Anath Rwebembera, alisema serikali imeendelea kufanya kazi na wadau katika kutekeleza afua mbalimbali za afya hasa katika uboreshaji wa miundombinu na utoaji wa huduma za afya.

Alisema serikali imejipanga kuhakikisha inafikia lengo la dunia la kutokomeza janga la UKIMWI ifikapo 2030 hivyo imeendelea kufanya kazi katika kuzifikia 95, 95, 95 ambazo zinatoa mwelekeo wa kufikia lengo kuu.

## HABARI KITAIFA



Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Tabora, Dk. Zainab Mango (wa tatu kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa shirika la Akili Platform Tanzania (APT), Roghat Robert (kulia) alipotembelea banda la shirika hilo, katika maadhimisho ya Wiki ya Sheria, mjini Tabora juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mshtuko kujiuzulu kwa Waziri Zanzibar

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale wa Zanzibar, Simai Mohamed Said, amejiuzulu kwa kile alichokisema ni kutokana na mazingira tatanishi ya kazi na yasiyo rafiki huku baadhi ya wanasiasa wakielezea kushtushwa na hatua hiyo.

Kutokana na hatua hiyo, Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu na Msemaji Mkuu wa Serikali Zanzibar, Charles Hilal, katika taarifa yake jana, alisema Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, amepokea barua ya kujiuzulu kwake na kuridhia uamuzi huo.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, Simai ambaye ni Mwakilishi wa Tunguu kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), alisema amewasilisha barua ya kujiuzulu kwa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi kutokana na mazingira magumu katika kutekeleza majukumu yake.

Ingawa hakutaja sababu za kujiuzulu, wachambuzi wa masuala ya siasa wamesema ni huenda ni kutokana na kuchoshwa na kuingiliwa mara kwa mara katika majukumu yake ya kila siku na watu walio karibu na Ofisi ya Rais.

Sababu nyingine, inadaiwa huenda ni kuchukizwa na uamuzi wa Bodi ya Vileo Zanzibar kuzinyanga'anya leseni kampuni tatu za kusambaza vileo na kuzipa kampuni zingine nje ya Zanzibar kuagiza vileo ambazo hazina uwezo, hivyo kusababisha upungufu wa bidhaa hizo visimwani humo.

"Ndugu wananchi, napenda kuwafahamisha kuwa nimemwandikia barua Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar kujiuzulu nafasi yangu kama Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale kuanzia leo (jana)... nimefikia uamuzi huu ambao hapa kwetu si rahisi katika utamaduni wetu," alisema.

Alisema kutokana na imani yake, jukumu namba moja la wasaidizi wa Rais, wakiwamo Mawaziri ni kumsaidia kutekeleza Ilani ya chama na inapotokea mazingira yasiyo rafiki, ni vyema kutafuta jawabu kwa haraka ili kazi ya kuwaletea wananchi maendeleo iendelee, ikibidi kukaa pembeni.

Hatua hiyo ya kujiuzulu, imekuja siku chache tu tangu alipotangaza kuwapo uhaba wa pombe Zanzibar unaathiri sekta ya utalii ambayo ndiyo nguzo kuu ya uchumi wa visiwa hivyo. Alisema kuwa si vyema sekta ya utalii ikachezewa kwa kuwa inachangia kwa kiasi kikubwa pato la taifa kutoa ajira kwa vijana wengi.

"Namshukuru sana Rais Dk. Mwinyi kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na hatimaye Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale. Nitaendelea kuwa mtiifu kwa serikali pamoja na chama changu, CCM." alisema.

Aidha, kujiuzulu kwa Simai kumetokea wakati kuna taarifa za mpasuko katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) ya Zanzibar.

Chama cha ACT Wazalendo kimekuwa kikilalamika kuwa kuna kukiukwa kwa makubaliano yaliyofikiwa kati ya Rais Dk. Mwinyi na na aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharrif Hamad (sasa marehemu) kuhusu kuundwa kwa serikali hiyo.

**MSHTUKO WANASIASA**

Baadhi ya wanasiasa Zanzibar, wameelezea kushtushwa na uamuzi wa waziri huyo kujiuzulu bila kueleza sababu.

Wakizungumza jana kwa nyakati tofauti, walisema kujiuzulu kwa Simai kuna madhara makubwa katika maendeleo ya utalii kutokana na uzoefu wake katika sekta hiyo.

Baraka Mohamed Shamte, mmoja wa wanasiasa hao, alisema amepokea kwa mshtuko kujiuzulu kwa waziri huyo lakini akasema hatua hiyo inaweza kuwa kuwa na sababu nyuma ya pazia kutokana na ukweli kwamba ni mmoja wa mawaziri wenye uhusiano makubwa na Rais Mwinyi kabla ya kushika wadhifa huo.

"Lazima kutakuwa na jambo limejificha. Sekta ya utalii imepoteza mtu muhimu kwa sababu Simai anaijua sekta ya utalii tangu ilipoazishwa na amewahi kutumikia sekta binafsi na serikali kabla ya kujiuzulu," alisema licha ya kuamini kwamba wako watu wanaoweza kushika wadhifa huo na kufanya vyema.

Mbunge wa zamani wa Kikwajuni, Parmuk Singh Hoogan, alisema uamuzi wa Simai kujiuzulu ni haki yake kidemokrasia lakini wananchi wanapaswa kuelezwa sababu za msingi alizozitoa kuchukua hatua hiyo.

Alisema inashangaza uwamuzi wake kujiuzulu umejitokeza siku chache tangu Zanzibar kukabiliwa na uhaba wa vileo (pombe), hivyo kuathiri sekta ya utalii visiwani humo.

"Waziri Simai alikuwa mtu anayeifahamu sekta ya utalii kwa sababu muda mrefu amekuwa katika katika sekta ya utalii kabla ya kuwa mwakilishi na baadaye Waziri, akitumikia muda mrefu katika Jumuiya ya Wawekezaji katika sekta ya utalii Zanzibar," alisema Hoogan.

Mmoja wa wakazi wa Unguja, Salum Hamza Sultani, alisema ameshangazwa na hatua ya Waziri huyo kijuuzulu kwani ni miongoni mwa mawaziri wachapakazi na ambao hawana kashfa yoyote ya ufisadi.

"Binafsi nimepata mshtuko kusikia amejiuzulu kwa sababu Simai ni kijana mwadilifu a na mchapakazi hodari na ambaye hana makuu. Ni Waziri anayetambua majukumu yake. Sasa sijui kimetokea nini," alisema.

Mkazi mwingine wa Unguja, Issa Omari Usi, alipongeza hatua ya kujiuzulu kwa Waziri huyo akisema inaonyesha ukomavu wake wa kisiasa na inaonyesha kwamba kwake kuwa Waziri ni kutoa huduma kwa wananchi na si kazi ya kujikimu kimaisha.

**-Imeandikwa na Rahma Suleiman, ZANZIBAR, na Joseph Mwendapole, DAR.**

# Wawili wafariki ziara Naibu Waziri Mkuu

**Na Hamida Kamchalla,**
TANGA

WATU wawili wamefariki dunia na wengine wawili kujeruhiwa baada ya gari walilokuwa wakisafiria kwenye msafara wa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko kupata ajali, alipokuwa katika ziara ya kikazi katika mkoa wa Tanga.

Ajali hiyo ilitokea jana majira ya saa 3:00 asubuhi katika kijiji cha Mamboleo, wilaya ya Muheza wakati msafara huo ukitokea jijini Tanga kwenda wilayani Korogwe kukagua mradi wa kufua umeme katika mji wa Hale.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Kamishna Msaidizi (ACP) Almachius Mchunguzi, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kuwataja waliofariki dunia kuwa ni Ally Hassan, mwandishi wa habari wa televisheni ya Halmashauri ya Jiji la Tanga (Tanga TV) na Saidi Alawi, dereva wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA).

Aidha, aliwataja majeruhi kuwa ni Frank Godfrey, mwandishi wa habari wa Ayo TV na Mhandisi wa Maji wa Tanga UWASA, Salum Ng'umbi, ambao wamelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Bombo.

"Gari hilo lilikuwa kwenye msafara wa Naibu Waziri Mkuu, ni mali ya mamlaka ya maji Tanga, aina ya Toyota Hilux lenye namba za usajili DFPA 9631. Gari hilo liliacha njia na kupinduka. Majeruhi wako hospitali ya Bombo wanaendelea kupatiwa matibabu," alisema.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Bombo, Dk. Frank Shega, alikiri kupokea majeruhi hao majira ya 4:00 huku akisema watatu walikuwa katika hali mbaya na mmoja alikuwa tayari ameshaaga dunia.

"Nimepokea majeruhi watatu na mwingine alikuwa ameshafariki dunia. Wakati wanapatiwa matibabu, mmoja naye akafariki dunia. Hali za majeruhi ni mbaya ambapo mmoja amesafirishwa kwenda Hospitali ya Taifa Muhimbili na mwingine alipelekwa chumba cha upasuaji,

"Huyu aliyepelekwa Muhimbili ni mhandisi wa maji Tanga UWASA, amepata tatizo la mifupa na mwingine mwandishi wa habari baada ya vipimo imeonyesha damu imemwagikia ndani, Madaktari wanaendelea kupigania maisha yake," alisema Dk. Shega.


VISIT
FREE ENTRY
INTL TRADE EXHIBITION ON AGRO & POULTRY - GRAINS
EXHIBITORS FROM AROUND 13 COUNTRIES
AGRO & POULTRY 2024
Intl Trade Show on Aquaculture, Agriculture, Dairy, Irrigation, Livestock & Poultry Tractors, Veterinary Etc.
Products on Display:
Poultry Feed Equipment | Poultry Silo | Feed Tankers | Feed Conveyor Storage | Feed Milling Systems | Metal Cutting | Poultry Slag | Feed Millilng Handling | Processing | Silos Poultry Cages & Equipment | Poultry & Dairy Construction Houses | Cage Systems | Egg Grading & Packing | Egg Printing System Feed System & Boilers | Layers Breeding | Animal Feeds & Flour Livestock Feed Supplement Raw Materials | Irrigation Lines | Fittings Equipments | Sprinklers | Vertical Planter | poultry Processing Equipment Slaughterhouse
Grains Africa 2024
International Grains & Technology Trade Exhibition
Products on Display:
Rice Milling Machines | Paddy Seperators | Grain Milling System Feed Milling Systems | Silos | Flour Mill Machinery | Facility-Corn Milling Facility | Semolina Milling | Mills | Feeds & Flour
Date & Venue
26-28 January 2024
Diamond Jubilee Hall, Dar-Es-Salaam - Tanzania
Timing
10:00 AM TO 6:00 PM
For more info, Please Call
0768 616 418 / 0656 482 557

# Anusurika kuuawa madai ya kuharibu mashine ya kamari

Na Tuntule Swebe

KIJANA ambaye jina lake halikufahamika mara moja, nusura apoteze maisha baada ya kuharibu mashine ya kuchezea kamari, maarufu kama dubwi au korokoro.

Kitendo hicho kilisababisha kushambuliwa na wananchi akidaiwa kuwa ni mwizi.

Mkasa huo ulitokea juzi usiku eneo la Tegeta Machinjioni, Dar es Salaam, nyumbani kwa mmiliki wa mashine hiyo, anayeuza vinywaji mbalimbali, aliyetajwa kwa jina moja la Mama Happy.

Mtuhumiwa huyo anayekadiriwa kuwa na miaka 30 hadi 40, alipigwa na kuumizwa sehemu mbalimbali kwa madai kuwa alicheza dubwi au kamari na kupoteza Sh. 30,000.

Walioshuhudia tukio hilo walidai alipatwa na hasira baada ya 'kuliwa' hela hizo na akaanza kutoboa mashine ili kutafuta pesa zake.

Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Tegeta Machinjioni, Salum Mketo, aliyefika eneo la tukio, aliiambia Nipashe kuwa kijana huyo alipigwa na wananchi waliosikia kelele za mwizi, baada ya Mama Happy kuomba msaada.

Hata hivyo, hakuthibitisha madai kuwa alikuwa amechomwa kisu na kupoteza damu nyingi.

"Baada ya kumshambulia ilibainika kuwa kijana huyo alibomoa korokoro hilo akilalamikia pesa zake lakini hakuwa mwizi kama ilivyodaiwa," alisema Mketo.

Mmoja wa mashuhuda, Ally Lugendo, alimlaumu Mama Happy kwa kuita wananchi wammalize kijana huyo akidai ni mwizi, akisema si uamuzi sahihi kukatisha uhai wa mtu na kujichukulia sheria mkononi.

Licha ya kulaumiwa mmiliki wa dubwi hilo alisisitiza kuwa kijana huyo lazima alipe mashine hiyo, akisema hajui gharama yake.

Hatibu Juma, mkazi wa Wazo, aliwaonya vijana kucheza mchezo huo kama hawana pesa na kwamba ni bahati nasibu, hivyo kuna kupata na kukosa.

Baada ya mkasa huo na vurumai zilizovuta watu wengi, Mketo alisema mtuhumiwa na Mama Happy, walipelekwa Kituo cha Polisi cha Wazo.

# Ghana kufungua kiwanda cha kuunganisa magari Tanzania

Na Romana Mallya

MAONYESHO ya Biashara ya Ghana Expo 2024 yanayofanyika mkoani Dar es Salaam, yamefungua fursa ya biashara, baada ya Ghana kuonyesha nia ya kufungua kiwanda cha kuunganisha magari nchini.

Akizungumza juzi katika ufunguzi wa maonyesho hayo, Ofisa Mkuu wa Biashara kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara ya Ghana, Kofi Addo, ambaye alimwakilisha Waziri wa Wizara hiyo, Kobina Hammond, alisema watakaporejea nchini mwao watakaa na kampuni ya magari ya Ghana ya Kantanka kuwaeleza hilo.

Alisema watawaeleza fursa iliyopo katika soko la Tanzania na pia kujadiliana na Wizara ya Uchukuzi ili kuona namna watakavyoingia katika soko hilo Tanzania.

Maonyesho hayo yanafanyika chini ya Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA) ambao ni utaratibu wa pamoja wa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika unalenga kuchochea uchumi na biashara miongoni mwa nchi wanachama.

Kwa ujumla lengo hilo litafikiwa kwa kufunguliana masoko ya biashara ya bidhaa na huduma kwa kuondoleana ushuru wa forodha na kulegeza masharti na taratibu nyingine zinazokuwa za kiushuru.

Akizungumza katika maonyesho hayo, Addo alisema: "Tutaanzisha kiwanda hiki kwa kulingana na mazingira kwa sababu tunatambua mazingira barani Afrika yanatofautiana. Tutazingatia hili pia, katika utengenezaji wa magari."

Kuhusu maonyesho hayo, alisema yanalenga kutambulisha bidhaa na biashara za nchini Ghana katika soko la Tanzania.

"Lakini pia yanalenga kuwaunganisha wafanyabiashara na kuongeza urari wa biashara kati ya Ghana na Tanzania," alisema Addo.

Naibu Balozi wa Ghana katika mataifa ya Afrika Mashariki, William Abochi, alisema ni muhimu kuwa na ushirikiano ili kuwezesha wafanyabiashara kuwa karibu na kukuza biashara na uchumi wa nchi hizo.

Pia alisema ziara ya wafanyabiashara wa Ghana nchini Tanzania imelenga kujifunza kutoka kwa wafanyabiashara wa Tanzania na kutafuta masoko nchini hapa.

Mwenyekiti wa Chemba ya Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC), Mercy Sila, alisema wameanzisha uhusiano kati ya nchi hizo ili kubadilishana uzoefu, kujifunza na kukuza biashara.

Silla alisema wanawake wapo tayari na wameanza kunufaika na uhusiano uliopo kati ya nchi hizo mbili.

Maonyesho haya ya siku tano pamoja na mambo mengine yanalenga kuimarisha uhusiano wa kiuchumi baina ya nchi hizi mbili ikiwa ni mikakati ya serikali kukuza biashara na mataifa mengine ya Afrika.


# MARUDIO YA TANGAZO/ NOTISI YA MNADA WA HADHARA

**LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD,** kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED**, tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mali/dhamana za mdaiwa wake kama ilivyo onyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya Siku saba (7) kama rudio la tangazo kuanzia tarehe ya Notisi /Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SALUM OMARI AMIRI | LATIFA M. MLANZI | HATI YA MAUZIANO ILIYOTOLEWA NA SERIKALI YA MTAA | UPEMBENI MWANDEGE, MKURANGA,MANISPAA YA ILALA | TAREHE NI KUANZIA 05/02/2024 NA KUENDELEA MUDA NI KUANZIA SAA 04;00 ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali iliyopo na mahali ilipo.
3. Mshindii wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyopungua 25% ya bei iliyofikiwa siku yamnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

**LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD P.O.Box 68172**
**Dar es Salaam, Tanzania**
**Tel: 0620 848 565/ 0714 598 559**
**Email: lehalelglc@gmail.com**

HABARI KITAIFA

# ADC yajivunia uchapakazi wa Queen Sendiga

**Na Halfani Chusi**

CHAMA cha Alliance for Democrat Change (ADC), kimemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuendelea kumtumia vyema Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, kwa kuamini kuwa ni hazina kwa nchi.

ADC imesema ndani ya muda mfupi alioutumikia umma, Sendiga ameonyesha kuwa ni kiongozi shupavu mwenye maono ya mbali asiyeyumbishwa.

Katibu mkuu wa ADC, Doyo Doyo, alisema jana kuwa uthubutu wake na namna anavyojenga hoja za kimaendeleo, ni msaada mkubwa kwa serikali.

"Mkoa wa Manyara umepata kiongozi shupavu. Naamini kwa uwezo wake, weledi na uchapakazi, atawafikisha mbali wananchi wa Manyara" alisema.

Doyo alimsifu kuwa sera na falsafa zake alizazinadi mwaka 2020 akiwa mgombea urais kupitia chama hicho, anazitekeleza kwa vitendo na ndizo zilizomtambulisha kwa muda mfupi katika siasa za Tanzania.

"Mwaka 2020 tulimpa dhamana Queen agombee kiti cha urais, falsafa zake za kuamini katika maendeleo ya jamii, kupambania usawa wa kijinsia, kutaka kuwakomboa Watanzania kupitia kilimo, elimu na afya ndizo anazozitekeleza kwa kiasi kikubwa mkoani Manyara.

"Tumeshuhudia anavyosimamia mabilioni ya fedha za umma katika elimu, miundombinu ya barabara na anavyovavutia wawekezaji kuingia mkoani Manyara. Ni wazi mwanamama huyu ni hazina kwa taifa letu," alisema.

Doyo alisema hata baada ya kushindwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, viongozi walioingia madarakani walivutiwa na siasa zake na ndiyo siri iliyozidi kumtangaza Sendiga katika ulingo wa siasa hadi sasa.

Katibu mkuu huyo alisema anaamini maono ya mwanasiasa huyo yatalifikisha taifa katika mafanikio makubwa endapo ataendelea kuaminiwa na viongozi wa juu.

Alisema kiongozi huyo ni mpenda ukweli asiyeyumbishwa katika kazi anapaswa kulindwa na kuaminiwa zaidi. Alisema chama chake kinajivunia kuwa na kiongozi wa serikali aliyetokana na chama chao na kwamba limekip-

# Makonda atwishwa zigo mikopo kausha damu

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WANANCHI wa Mkoa wa Singida wamewasilisha kilio kwa Katibu wa Halmashauri kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Paul Makonda, kutaka chama kiingilie kati kutokana na taasisi zinazotoa mikopo 'chap chap' yenye riba kubwa, maarufu kausha damu, kwa unyanyasaji na udhalilishaji wanaofanyiwa na kusababisha kuvunjika kwa ndoa nyingi.

Malalamilo hayo yaliwasilishwa jana kwa Makonda wakati akizungumza na wananchi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika viwanja vya stendi ya zamani mjini Singida. Makonda alitumia muda huo kuwapa fursa ya kueleza kero zinazowakabili.

"Hali ni mbaya ndani ya familia zetu hatukai kwa amani. Wale wa mikopo ya kausha damu wanakuja kuchukua kabati, vitanda, makochi na magodoro. Je, hapo kuna ndoa? Tunaomba serikali irudi ikae chini iwaangalie watoa mikopo hii ambao wanakuja na mgambo," alisema Shaban Selema ambaye alijitambulisha kuwa ni Mwenyekiti wa Mkoa wa Singida wa Shirika la Wanaume Wanaopitia Changamoto za Ndoa.

Kutokana na malalamiko hayo, Makonda alimwita Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, ambaye alikuwapo kwenye mkutano huo aeleze wananchi kama wenye taasisi za mikopo ya kausha damu wana leseni.

Pia aliuliza ni nani ,anayepanga hesabu za riba na kama serikali inapata kiasi gani kw aroba hizo.

Waziri Mwigulu akijibu malalamiko hayo, alisema watu wanaotoa mikopo ya kausha damu walipewa leseni na riba wanayopata inakuwa yao na si wizara wala waziri anayepata chochote kwenye riba.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani, alimwelekeza Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na idara inayosimamia taasisi ndogo za kifedha ndani ya Wizara ya Fedha kupitia upya masharti ya utoaji leseni ambazo taasisi hizo zinatumia vibaya na kuweka riba kubwa kwa wateja.

"Watu wanatumia vibaya leseni kuweka riba wanazojipangia. Zingine zilikuwa mara asilimia 50, 100 hadi 200 na hii si kwa wananchi hata watumishi wa umma wamo kwenye kilio hicho," alisema.

Dk. Nchemba alisema kwa sasa leseni zote zimepitiwa upya na zinatolewa kwa masharti yanayokuwa na wigo ambao uko chini kama ambavyo benki zinatoa.

"Hivi sasa ziko leseni ambazo zimeshafutwa kwa sababu kutoza riba kubwa ambazo hazina ubinadamu ndani yake na unyanyasaji. Kuna baadhi ya kausha damu wana mahabusu zao na mtu akifika hapo wanamweka ndani kinyume cha taratibu," alisema.

Waziri huyo alisema kama bado zipo taasisi za mikopo ambazo zinaendelea kutoa mikopo ya kudhalilisha wananchi wafike katika ofisi za wakuu wa mikoa kutoa taarifa ili serikali iweze kuchukua hatua haraka za kisheria.

Makonda alisema kuna mambo mengi yamekaliwa kimya lakini yanawaumiza wananchi na kutokana na hali hiyo, Rais baada ya kumteua, alimpa mambo 10 ya kuyafanya kuwatumikia wananchi.

Kuhusu kilimo, alisema inashangaza maofisa ugani licha ya kupewa pikipiki, vishikwambi na vifaa vya kupimia udongo bado wako mjini wanakula kiyoyozi.

Makonda alitoa miezi mitatu kwa Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kutoa ripoti kujua kila kijiji kama ofisa ugani aliyeajiriwa yuko kwenye kituo chake cha kazi na kama yuko Mkurugenzi wa Halmashauri ambaye hatoi mafuta kwa ofisa ugani, chama kijulishwe ili hatua zichukuliwe.




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko akiwasha umeme katika kijiji cha Kigandini, wilayani Mkinga mkoani Tanga juzi. Kushoto ni Mbunge wa Mkinga ambaye pia ni Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Dunstan Kitandula. **PICHA: WN**

# Biteko: Rais anakerwa viongozi kutotatua matatizo ya wananchi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amesema Rais Samia Suluhu Hassan anataka kuona viongozi wote wanatatua kero na changamoto za wananchi.

Kutokana na azma yake hiyo, Biteko amesema Rais anasikitishwa na baadhi ya viongozi ambao hawatatui changamoto za wananchi mpaka paleanapofanya ziara katika maeneo mbalimbali nchini.

Dk. Biteko alisema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi katika vijiji vya Magodi na Kigandini, Mkinga mkoani Tanga baada ya kuwasha umeme katika vijiji hivyo ambao umesambazwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Katika ziara yake kwenye Vijiji hivyo, Dk. Biteko aliambatana na Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba, Mbunge wa Mkinga ambaye ni Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Dunstan Kitandula na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba.

"Mheshimwia Rais anafanya kazi kubwa katika kila sekta na mabilioni ya pesa yamekuwa yakipelekwa kila mkoa kwa ajili ya kuboresha huduma kwa wananchi.

Nikitolea mfano hapa Tanga, serikali imeshatoa Sh. trilioni 2.6 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kwenye umeme miradi inaongezeka kwani mmepata Sh. bilioni 133.6 huku wilaya ya Mkinga ikipata Sh. bilioni nane kwa ajili ya usambazaji umeme. Dk. Samia anapambana ili kuwaletea maisha bora Watanzania, hivyo viongozi wengine tusiishie kusikiliza kero tu bali tuzitatue na kama kuna mahali tunahitaji watupe muda, tuwaambie kwa uwazi," alisema.

Katika hatua nyigine, Dk. Biteko aliwataka wazazi na walezi nchini kuwapeleka shuleni watoto wote wanaostahili kuwa shuleni katika kipindi hiki ambacho shule zimefunguliwa ili wapate elimu itakayowasaidia katika maisha yao na nchi kwa u umla. Alisema katika mkoa wa Tanga, watoto walioripoti Shule ni asilimia 60 tu.

Kutokana na hali hiyo, aliwaagiza viongozi kusimamia suala hilo ikiwamo kuendesha msako na kutumia sheria zilizopo kwa wale wanaoficha watoto ili wasiende shule kwa kuwa ifikapo Machi, watoto wote wanatakiwa wawe wameripoti shuleni.

Kuhusu usambazaji umeme vijijini, alipongeza REA kwa kuendelea na kazi hiyo akitolea mfano kuwa usambazaji umeme vijijini mkoani Tanga umefanyika kwa asilimia 91 na wilaya ya Mkinga yenye vijiji 85, tayari 82 vimesambaziwa umeme huku kazi ya kusambaza kwenye vijiji vilivyosalia ikiendelea na baadaye vitafuata vitongoji.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maandalizi AFCON 2027 yaanze mapema ili tusiwe wasindikizaji

**FAINALI** za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), bado zinaendelea kurindima huko nchini Ivory Coast wakati hatua ya 16 Bora ya michuano hiyo itakayomalizika Februari 11, mwaka huu ikitarajiwa kuanza leo.

Baada ya kumalizika kwa mechi za hatua ya makundi, michezo ya 16 Bora itakuwa ni kati ya Nigeria dhidi ya Cameroon wakati Angola watawavaa Namibia, Cape Verde yenyewe itachuana na Mauritania huku Waarabu wa Morocco wakiwaalika Afrika Kusini.

Mali itashuka dimbani kucheza dhidi ya Burkina Faso, Misri itakutana na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) huku Equatorial Guinea itapambana dhidi ya Guinea na wenyeji, Ivory Coast watawakaribisha mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Senegal.

Timu ya Soka ya Tanzania (Taifa Stars), ni moja ya timu zilizoishia hatua ya makundi wakiwamo vigogo Algeria, Tunisia, Msumbiji, Zambia, huku Ivory Coast wakisonga mbele kupitia tundu la sindano.

Taifa Stars ambayo mwaka huu ilikuwa inashiriki fainali hizo kwa mara ya tatu, imeondoka katika michuano hiyo ikivuna pointi mbili, baada ya kupata sare dhidi ya Zambia na DRC, huku ikiambulia kichapo cha mabao 4-0 katika mchezo wake wa kwanza ilipokutana na Morocco.

Ukurasa wa michuano hiyo iliyoanza Januari 13, mwaka huu umeshafungwa na wakati wowote kikosi cha Stars kitarejea nchini kwa ajili ya wachezaji kurejea katika majukumu ya kuzitumikia klabu zao.

Lakini kumalizika kwa fainali hizo, ndio kuanza rasmi kwa maandalizi ya kuelekea michuano ijayo ambayo itafanyika mwakani, lakini pia ile itakayofanyika mwaka 2027, Tanzania, Kenya na Uganda tukiwa wenyeji.

Kupitia fainali za mwaka huu, Idara ya Ufundi ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), ina mambo mbalimbali mazuri ambayo imejifunza, inatakiwa kuyachukua na kuyahamishia kwenye kikosi cha Stars ili kupata matokeo chanya katika mechi zinazofuata za kusaka tiketi ya kufuzu.

Idara ya Ufundi ya TFF inatakiwa pia kuyaboresha yale mazuri yaliyofanywa na wachezaji wetu kwa ajili ya kuwaongezea ujuzi na hatimaye kuwa na kikosi chenye ubora kuelekea katika fainali zijazo.

Ni jambo la wazi katika fainali za mwaka huu, kikosi cha Stars kimeonyesha mabadiliko makubwa tofauti na kilivyokuwa kwenye michuano iliyopita, hii ni dalili njema kwa Tanzania endapo mazuri yataboreshwa na hatimaye tutarejea katika mashindano mengine timu ikiwa 'moto'.

Stars ambayo ilizoeleka ikitumia wachezaji wengi wanaocheza soka hapa nyumbani, iliingia katika fainali za AFCON mwaka huu ikiwa na sura mpya, ingawa idadi kubwa ya nyota wanaosakata kandanda ughaibuni hawakucheza, lakini tunaamini walikuwa na mchango na waliongeza ushindani kwenye mazoezi kwa ajili ya makocha kupata kikosi cha kwanza.

Nyota hao wanatakiwa kuendelea kuwapo ili kuongeza vita ya namba lakini pia waliopata nafasi ya kupeperusha bendera ya Tanzania, hawatakiwi kubweteka na badala yake wajiimarishe kwa sababu tunahitaji kuonyesha ushindani na kutokuwa wasindikizaji kwenye fainali zinazofuata.

Hakuna kisichowezekana, kama Stars imefanikiwa kuvuna pointi mbili kutoka kwa Zambia na DRC, zinazoundwa na nyota wanaocheza kwenye ligi ngumu Ulaya, bado inaweza kufanya vyema katika mashindano yajayo na kuiweka Tanzania kwenye ramani mpya.

TFF kwa kushirikiana na serikali inatakiwa kuipatia Stars michezo mbalimbali ya kirafiki dhidi ya vigogo ili kuwajenga wachezaji na kuwaweka tayari kuvaana na nyota wenye viwango vya juu, na kwa kufanya hivyo, matokeo yake yatasaidia kuwanyanyua nyota wetu.

Tunapenda kutumia nafasi hii kuwakumbusha wachezaji wote watakaopata nafasi ya kuitwa katika kikosi cha Stars kuongeza umakini na utulivu katika kutekeleza majukumu vizuri.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Stars isibezwe, imefanya vyema ikilinganishwa AFCON zilizopita

Na Adam Fungamwango

**NI** kweli, Timu ya Soka ya Taifa ya (Taifa Stars), imetolewa katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), kwenye hatua za makundi.

Stars imeshika nafasi ya mwisho katika msimamo wa Kundi F kwenye kinyang'anyiro cha fainali hizo zinazoendelea nchini, Ivory Coast.

Kama kawaida ya Wabongo, kumekuwa na kelele nyingi za kwa nini Taifa Stars haikufuzu kwenda hatua ya 16 bora.

Wengi wanasema kwa namna kundi lilivyokuwa, timu iliyokuwa inaogopesha ni Morocco tu, na si Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) au majirani Zambia (Chipolopolo).

Wengine wakaenda mbali kwani baada ya kuiona Morocco, wakadai nayo vile vile haikuwa katika kiwango cha kutisha na bila kadi nyekundu ya Dismas Novatus, basi mechi ingeweza kumalizika kwa sare ya kufungwa idadi ndogo ya mabao na si 3-0 kama ilivyokuwa.

Lawama na Watanzania wengi ni kile walichokiita uzembe uliofanywa katika mechi dhidi ya Zambia na kuruhusu warudishe bao dakika tatu za mwisho wakati ikiongoza 1-0.

Ni mechi ambayo ilionekana kama Stars ingeshinda na kupata pointi tatu, halafu ikatoka suluhu kama ilivyofanya dhidi ya DR Congo, moja kwa moja saa hizi Tanzania ingekuwa bado ipo katika fainali hizo, pia ingeweka rekodi mbili kwa pamoja, kushinda mechi kwa mara ya kwanza kwenye historia ya michuano hiyo na kutinga hatua ya 16 bora.

Wakati michuano hiyo ikianza niliandika tusiipe timu matarajio makubwa kwa sababu inaonekana kabisa bado 'inajitafuta'.

Ukweli tu usemwe baada ya kushiriki fainali za kwanza mwaka 1980, Taifa Stars ni kama ilipoteza kabisa mwelekeo wa kisoka na hadi ilipokuja kutinga mara ya pili baada ya kupita miaka 39.

Kutoka 2019, imetumia miaka michache tu kurejea tena kwenye fainali hizo, kama huko nyuma ingeweza kufanya hivyo saa hizi tungekuwa tunaongea suala ya timu kufika robo fainali na siyo kuweka rekodi ya kushinda kwa mara ya kwanza ambayo imetushinda tena kwa mara nyingine.

Pamoja na yote hayo, Stars inaonekana kuna kitu imekiongeza kwenye fainali za mwaka huu.

Katika mechi zote tatu inaonekana wachezaji wanapambana sana, tatizo linabaki pale pale uwezo wao unakuwa umefikia pale.

Kazi iliyobaki sasa ni kwa wale waliobaki, kuwatafutia au kuwatengenezea vijana watakaokuwa na viwango vya juu kidogo zaidi ya hawa waliopo.

Licha ya kushika mkia na kutoshinda mechi yoyote, lakini Stars hii imeweka rekodi ya juu zaidi kuliko zile mbili zilizopita kitakwimu.

Imemaliza ikiwa na pointi mbili, ikiipiku ile iliyofuzu 1980, ambayo ilimaliza ikiwa na pointi moja tu, achilia mbali ya 2019 ambayo haikupata pointi yoyote.

Stars hii iliyokuwa Kundi F imepata sare mbili kwa mara ya kwanza, ikitoka bao 1-1 dhidi ya Zambia na suluhu dhidi ya DRC, ambapo ya 1980 ilimaliza ikiwa na sare moja, huku iliyopita ikipoteza mechi zote tatu.

Kwa kuwasaidia zaidi vijana wa sasa ni, Stars ya mwaka 1980 iliyokuwa Kundi A fainali zikichezwa Nigeria ilianza kwa kufungwa mabao 3-1 na mwenyeji halafu ikafungwa magoli 2-1 dhidi ya Misri na mechi ya mwisho ikatoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Ivory Coast.

AFCON ya 2019 iliyochezwa Misri, ilianza kwa kuchapwa mabao 2-0 dhidi ya Senegal, ikapoteza mabao 3-2 dhidi ya Kenya (Harambee Stars), na ikamaliza na kipigo cha mabao 3-0 dhidi ya Algeria.

Hiyo inaonyesha kuwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Ivory Coast ndiyo matokao makubwa zaidi mazuri ya Stars.

Safari hii Stars imepata sare mbili, hivyo imevunja rekodi ya fainali mbili zilizopita.

Pamoja na Watanzania wengi walitaka rekodi ya angalau kushinda mechi ya kwanza, lakini imeshindikana, ila rekodi hii nayo pamoja na viwango vya wachezaji wetu vinatia matuaini ya kufanya vizuri zaidi AFCON ya 2025 itakayochezwa Morocco na ile ya 2027 itakayopigwa Tanzania kwa kushirikiana na Uganda na Kenya.

Kinachohitajika ni uvumilivu tu, nimaamini fainali hizi zinapomalizika, kila kitu kwa Stars kinabaki kuwa historia.

## Utafiti kuwanufaisha wajasiriamali wadogo

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe, Prof. William Mwegoha, amesema utafiti mbalimbali unaofanywa na wanataaluma wa chuo hicho umelenga kuwainua vijana wa Kitanzania kwa kuwapatia mitaji kupitia uchangiaji wa umati.

Prof. Mwegoha alisema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa kongamano la kimataifa linalofadhiliwa na serikali ya Denmark kupitia mpango wa kutumia michango ya umati kuwezesha wajasiriamali wadogo nchini (C4YET ) lililofanyika jijini Arusha.

Alisema utafiti huo katika masuala mbalimbali unalenga kuangalia mbinu mbalimbali, faida kwa mlengwa na mchangiaji ili kuwainua vijana na wajasiriamali wadogo kupitia uchangiaji huo.

"Kwa chuo chetu Mzumbe ni utafiti wenye manufaa makubwa kwa sababu unachangia kwenye dhana ya serikali ya kuhakikisha wajasiriamali wadogo wanawezeshwa mitaji," alisema Prof. Mwegoha.

Alisema kupitia kongamano hilo linalowakutanisha wataalamu kutoka vyuo mbalimbali vikiwemo Mzumbe na Chuo Kikuu cha Copenhagen kutoka Denmark, watafiti watabadilishana matokeo ya utafiti na kupata njia sahihi ya kutekeleza dhana ya uchangiaji wa umati.

Prof. Mwegoha amesema mradi huo ulianza mwaka 2019 na ni wa miaka mitano ambao umewanufaisha vijana wa maeneo yote ya mijini na vijijini.

Naye Mratibu wa Mradi huo, Dk. Nsubili Isaga, kutoka Shule ya Biashara ya Chuo Kikuu Mzumbe, alisema mradi huo umewainua wajasiriamali kutokana na kubuni nyenzo walizotumia za uandishi wa andiko lililowavutia wafadhili kwa ajili ya wanataaluma kusaidia utafiti na hatimaye chuo kushirikisha SIDO kuwakwamua wajasiriamali vijana kwenye mikoa ya Arusha, Mwanza, Dar es Salaam, Morogoro na Mbeya.

Aliongeza kuwa wajasiriamali 187 walipewa mafunzo hayo na 100 kati yao walipata mikopo yenye riba ya asilimia tano tu inayowawezesha kuirejesha kwa wakati na baadaye vijana wengine watafikiwa zaidi ili wajiunge na majukwaa ya biashara mitandaoni.

# Maabara TBS zapata vyeti umahiri

**Na Joseph Mwendapole**

MAABARA zote nane za Shirika la Viwango Tanzania (TBS) zimepata vyeti vya umahiri vinavyozifanya zitambulike kimataifa, ambapo maabara mbili za nguo na ngozi na Maabara ya Kituo cha Ufungashaji zimepata vyeti hivyo kwa mara ya kwanza.

Vyeti hivyo vilivyotolewa na Shirika la Huduma za Ithibati za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADCAS) ni uthibitisho kwamba maabara hizo zinatambulika kimataifa na matokeo ya vipimo vyake yanatambulika kimataifa.

Hafla ya kukabidhi vyeti hivyo vya umahiri kwa maabara hizo ilifanyika jana jijini Dar es Salaam.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Kaimu Mkurugenziwa Mkuu wa TBS, David Ndibalema, alisema SADCAS ilifanya tathmini kwenye maabara za shirika kulingana na kiwango cha kimataifa na wametoa vyeti vya umahiri ambavyo vinathibitisha umahiri wa hizo maabara.

"Vyeti hivi vinaongeza wigo wa maabara zetu zenye vyeti hivyo, kwani tulikuwa na maabara sita na sasa zimeongezeka mbili, maabara ya nguo na ngozi na maabara ya kituo chetu cha ufungashaji," alisema Ndibalema.

Alisema vyeti hivyo ni uthibitisho kwamba huduma wanazotoa za upimaji kwenye maabara za TBS zinatambulika kimataifa na kwamba kupata vyeti hivyo vya umahiri kunajenga imani zaidi kwa wateja, ambao wanafika kupata huduma za upimaji mmoja mmoja.

Ndibalema alisema vyeti hivyo vinajenga imani kwa wale wanaowapatia huduma za kutoa ithibati ya ubora na inakuwa rahisi vyeti vyao wanavyotoa na majibu ya maabara wanayotoa yanatambulika kimataifa na hivyo kuwezesha biashara ndani ya nchi na nje nchi.

"Kama wote tunavyotambua Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo ushirikiano wetu umejikita zaidi katika kukuza biashara katika hizo nchi lakini sisi ni wananchama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na ni wanachama wa Umoja wa Afrika (AU). Katika ngazi ya Afrika, tuna soko huru la biashara , kwa hiyo kupata vyeti vya umahiri katika maabara zetu za upimaji ni hatua mojawapo ya kurahisha bidhaa zetu kushindana katika masoko hayo," alisema Ndibalema.

Alisema hiyo ni kwa sababu majibu ya maabara na vyeti wanavyotoa vitakuwa vinatambulika na hivyo kukubalika katika masoko hayo na hiyo itasaidia bidhaa za Tanzania kupata msoko na kutambuliwa na taasisi zingine za udhibiti katika Kanda ya Afrika.

Naye Mkurugenzi wa Upimaji na Ugezi wa TBS, Ridhiwan Matange, alisema jana ilikuwa siku muhimu kwa kurugenzi yake anayoisimamia ambapo sasa maabara zote nane zimepata vyeti vya umahiri.

"Maabara sita kati ya nane zilishapata vyeti vya umahiri na sasa maabara zingine mbili zimeongezeka na kupata vyeti vya umahiri na sasa maabara zote chini ya Kurugenzi ya Upimaji na Ugezi zimepata vyeti vya umahiri.

"Ni jambo muhimu sana ambapo wote tunastahili kujivunia mafanikio haya, kwani mchakato wa kupata vyeti hivi sio kazi ya siku moja, inahitaji uwekezaji kwa maana ya rasilimali watu, kuwapatia ujuzi, kuwa na vifaa vya kisasa, mazingira bora ya upimaji na pamoja na hatua zingine za upimaji," alisema.

Alisema Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Yusuf Ngenya, na menejimenti wamewekeza vya kutosha kuhakikisha wanaweza kufikia malengo hayo, kwani kufikia hatua hiyo inahitaji uwekezaji na utashi wa menejimeti.

Naye Kaimu Mkuu wa Maabara ya Nguo na Ngozi, Habib Hamis, alisema kwa kupata cheti cha umahiri inawasaidia kwa namna mbili, moja kufahamika kimataifa kwamba ina uwezo wa kupima na kutoa majibu ambayo yanatambulika kimataifa na pili inaitambulisha TBS kwamba ina maabara ambayo inaweza kupima na majibu yake yanambulika kimataifa.

Alishauri wazalishaji ndani ya nchi na waagizaji nje ya nchi wafike TBS kwa ajili ya kuhakiki ubora wa bidhaa zao.



Wanafunzi wa shule ya sekondari ya Feza Boys, wakishangilia huku wakiwa wamemnyanyua juu mhitimu wa kidato cha nne William Fredrick, aliyefaulu kwa kupata daraja la 1.7, baada ya kupata matokeo ya kidato cha nne ambapo shule hiyo imeongoza kufaulisha wanafunzi wote 76 kwa kupata daraja la kwanza, wakati wa hafla ya kuwapongeza shuleni hapo, Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DED apewa kibano madirisha ya shule

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa**
MANYARA

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, amempa siku tano Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang, Francis Namaumbo, kulipa deni la Sh. milioni 27.5 kwa vijana waliotengeneza madirisha ya shule.

Agizo hilo alilitoa juzi baada ya vijana hao kutoa malalamiko yao mbele ya Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, wakati akizungumza na wananchi wa mji mdogo wa Katesh Wilaya ya Hanang akiwa njiani kwenda mkoani Singida.

"Vijana wana haki kwa namna nilivyosikiliza malalamiko na majibu ya Mkurugenzi wetu, hivyo naomba nikuhakikishie kama serikali ilifanya ubovu wa kutia saini hati mbovu na ubovu huohuo wautumie kuwalipa pesa zao vijana hawa.

Namwagiza Mkurugenzi kuhakikisha ndani ya siku tano ifikapo Januari 30, fedha hizo ziwe zimelipwa zote," alisema Sendiga.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Timoth Carol, alisema walifanya kazi ya kutengeneza madirisha ya shule yenye thamani ya Sh. milioni 27.5 na mhandisi wa halmashauri ya wilaya alishawapatia hati ya kuonyesha kumalizika kwa kazi tangu Septemba, mwaka jana lakini hawakumlipa.

Alisema viongozi wa serikali baada ya kusikia Makonda ana ziara katika mkoa, akaitwa na kupelekwa kwenye mradi na kuambiwa hakuna ubora wa kazi aliyoifanya na kujulishwa atalipwa Sh. milioni 13.5 jambo ambalo hakukubaliana nalo.

Caros alisema vifaa alivyotumia katika mradi huo alikwenda kukopa na baadhi ya mmoja anayemdai alimtishia kumpeleka polisi huku ofisi ya mkurugenzi ikiendelea kumzungusha.

Awali, mkurugenzi huyo, alisema kazi hiyo hakuifanya kwa ubora unaotakiwa kwa kuwa baadhi ya taasisi za serikali ziliwajulisha madirisha hayo yametengeezwa chini ya viwango na kuwataka wayarekebishe.

Makonda baada ya kusikiliza, alibaini makosa ndani ya ofisi ya mkurugenzi na kuhoji kama vijana hao walifanya kazi chini ya ubora iweje wapewe hati ya malipo ya ya Sh. milioni 27.5 wakati ingetakiwa ionyeshe sh. milioni 13.5.

Alisema hata malipo ya Sh. milioni 13.5 wameendelea kuwazungusha jambo ambalo ni kuwanyima haki zao kwa kuwa wamedai bidhaa walizotumia katika ujenzi huo walikwenda kukopa.

"Tunawezaje kuwajengea uchumi vijana wa nchi yetu kama iwapo hata kazi wanazofanaya kwenye serikali yetu na bado hamuwalipi? Rais Samia Suluhu Hassan anawapenda vijana na kuwaamini kufanya hivi ni kumkosea na kuwanyima haki vijana wetu," alisema Makonda.

Makonda amewaagiza wakurugenzi kuacha kuwstumia maofisa kilimo kama wakussnyaji wa mapato katika Halmashauri zao badala ya kuwafuata wakulima mashambani, kutoa elimu ya kilimo.



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda (wa pili kushoto), akikabidhi begi la shule kwa mmoja wa wanafunzi kutoka familia zenye uhitaji, wanaosoma katika shule za msingi za tarafa ya Chamriho, wilayani Bunda juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania yaanza utekelezaji wa mradi uhifadhi matumbawe

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) imeanza utekelezaji wa mradi wa uhifadhi wa matumbawe unaofadhiliwa na Shirika la Global Fund.

Mradi huo unatekelezwa na nchi sita ikiwamo Tanzania, zilizo katika mwambao wa Magharibi mwa Bahari ya Hindi.

Tanzania imepatiwa Dola za Marekani 900,000 sawa na Sh. bilioni 450, ili kutekeleza mradi huo kwa miaka minne iliyoanzia Machi 2023.

Mkuu wa Uhifadhi MPRU ambaye ni Msimamizi wa Mradi huo, Godfrey Ngupula, aliyasema hayo mwanzoni mwa wiki jijini Dar es Salaam katika mkutano ulikutanisha wadau mbalimbali wa bahari ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wake.

Katika mkutano huo, wadau hao walipata fursa ya kuandaa mpango kazi ili kusaidia matumizi ya maeneo ya matumbawe katika bahari yanainufaisha nchi kiuchumi na kuweka mazingira endelevu kwa utunzaji wa samaki na viumbe bahari.

Ngupula alisema moja ya maeneo ya bahari yaliyovamiwa ni pamoja na matumbawe ambayo yameathiriwa na shughuli za kibinadamu na mabadiliko ya hali ya hewa.

Alisema kuna nafasi kubwa imeachwa kati ya wataalam, wananchi, wanaosimamia sheria na sera. "Mradi huu kwa ujumla umelenga kujenga uelewa kuhakikisha elimu ambayo wataalam wanayo, hawa wa chini ambao ndio watumiaji wa haya matumbawe waipate.

"Pia watunga sera na wanaosimamia sheria nao wapate uelewa, wajue faida za kuyatunza wajue yakiharibika nini kitatokea. Lakini tukitunza nini faida tunazozipata kama nchi," alisema.

Alikumbusha kuwa matumbawe ambayo yapo Tanzania hayapatikani sehemu nyingi, kwa kuwa ni aina ambayo inastahimili hali ya hewa.

"Haya matumbawe yanaanzia toka nchi ya Msumbuji yanakuja Mtwara, Rufuji, Kibiti, Kilwa, Mafia, Tanga mpaka Pemba. Haya kwenye bahari yetu tunasema ni maeneo ya uzalishaji mkubwa sana wa mazalia ya samaki.

"Kama mnafahamu, serikali imejenga bandari ya samaki Kilwa ni kwa sababu ya maeneo haya. Kwa nini tunapata samaki wengi Kilwa? Ni kwa sababu ya matumbawe.

"Tumewalika wataalam mbalimbali wakiwamo wananchi na wasimamizi wa haya maeneo ili wote tuseme faida za matumbawe tunazifahamu, nini kifanyike kutokana na hali inayoendelea ili rasilimali iweze kutufaa sisi na kizazi kijacho," alisema.

Akifafanua kuhusu fedha za mradi huo, alisema Tanzania inatekeleza kwa Dola 900,000 ambapo kwa mwaka wanapata Dola karibia 37,000 na unatekelezwa kwa miaka minne ukianza Machi 2023 na kutarajiwa kuisha 2027.

Kaimu Meneja MPRU, Davis Mpotwa, alisema moja ya shughuli MPRU wanazofanya ni kuhakikisha shughuli za bahari zinatumika kwa namna ambayo ni endelevu.

"Lengo la mpango huo ni kuwapo kwa matumizi sahihi ya bahari kulinda matumbawe ambayo ni sehemu ya mazalia ya samaki, yanasaidia kuweka hali nzuri ya oksijeni katika maji.

"Ni sehemu ya utalii wa baharini, watalii wengi wanapokuja nchini wanazamia na kutazama bustani za matumbawe," alisema.

Alisema mpango kazi utasaidia kuhakikisha matumizi ya maeneo yao hususan matumbawe katika maeneo ya bahari yanasaidia Tanzania kiuchumi na hali ya utunzaji samaki na viumbe vya baharini inakuwa endelevu.

"Matumbawe yana mchango mkubwa katika kuhakikisha uchumi wa buluu unakua katika nchi yetu.

"Kwa ujumla kikao hiki kitatoka na maridhiano yatakayosaidia wadau walipo katika mwambao wa nchi nzima kuhakikisha matumbawe yanatunzwa kwa ajili ya taifa.

"Kwa ajili ya uchumi na kipato cha kila mwananchi, na kusaidia dunia nzima kuhakikisha mazingira yanatunzwa kwa hali endelevu," alisisitiza.

Alisema maazimio ya mkutano huo yatawasaidia kuhakikisha wanaendeleza juhudi nyingine yakiwamo maeneo ambayo yameharibiwa kurejeshwa na wale wanaotumia maeneo ya bahari kutumia kwa njia salama.

Alisema kuwa maeneo yaliyotengwa Tanzania kama hifadhi kuwa ni matatu; Hifadhi ya Bahari Silikanti Tanga, Hifadhi ya Bahari ya Guba ya Mnazi (Mnazi Bay), Mtwara na Hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafia na maeneo tengefu.

Mpotwa alisema sehemu kubwa ya samaki Dar es Salaam wanaopatikana feri na kwingine, hutoka katika mwamba uliopo kisiwa cha mnyororo.

"Ukuaji wa mazao ya uvuvi utasaidia taifa kuongeza pato pamoja na mtu mmoja mmoja. Unapotupa taka una athiri bahari una athiri utalii na viumbe vilivyopo chini ya bahari.

"Tunafanya kazi kubwa na wadau kwa kuzamia chini ya bahari kutoa taka za plastiki zinazonasa katika matumbawe na kusafisha fukwe,"alisema.

Msimamizi wa Miradi ya Pwani na Bahari kutoka Shirika Kimataifa la Uhifadhi wa Mazingira (WWF) Tanzania Dk. Modesta Medard, alisema mradi wa kulinda matumbawe uliandaliwa mwaka 2020/21 kwa kushirikiana na nchi nyingine sita za visiwa vya Magharibi Bahari ya Hindi.

Alisema mwezi Desemba 2021 walipata fedha Dola za Kimarekani milioni 7.848 zilizogawanywa katika nchi hizo sita.

"Hifadhi ya bahari inayosimamia maeneo tengefu nimepata dhamana ya kutekeleza na kusimamia mradi huu.

"Kwa hiyo, sisi WWF kazi yetu imekwisha, kazi iliyobaki ni kutoa ushauri wa kitaalam. Sisi pamoja na serikali tukaona mradi uende MPRU kwenye hifadhi ya bahari wausimamie na kutekeleza ni wa miaka minne," alisema.

# Watanzania wapelekwa kushika uongozi migodi nje

**Na Faustine Feliciane, aliyekuwa** KAHAMA

UONGOZI wa Kampuni ya uchimbaji madini ya Barrick umeanza mchakato wa kupeleka Watanzania kushika nyadhifa mbalimbali kwenye migodi ya kampuni hiyo nje ya nchi.

Barrick kwa nchini, inamiliki kwa ubia na Serikali migodi ya North Mara mkoani Mara na Bulyanhulu Shinyanga.

Akizungumza mkoani Shinyanga kwenye mgodi wa Bulyanhulu wakati wa kuwasilisha ripoti ya utendaji yo robo mwaka, Rais na Mtendaji Mkuu wa Barrick, Dk Mark Bristow, alisema hatua hiyo ya kuwapa nafasi Watanzania kwenye migodi inayomilikiwa na kampuni hiyo nje ya nchi ina lenga kuwaongezea ujuzi na uzoefu kwenye sekta ya uchimbaji madini.

"Nimefurahishwa sana na mazingira ya uwekezaji chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, na hii imepelekea sasa kupeleka Watanzania kwenda kupata ujuzi zaidi wa uendeshaji wa migodi katika migodi yetu nje ya Tanzania," alisema Bristow.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuwa na wataalamu wengi Watanzania kwenye sekta ya uchimbaji madini watakaosaidia kuendeleza sekta hiyo.

Barrick inamiliki migodi ya uchimbaji madini katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Ivory Coast, Chile, Marekani, Canada, Argentina na Jamhuri ya Dominica.

Akizungumzia hatua hiyo, Naibu Waziri wa Madini, Dk Steven Kiruswa, alipongeza hatua hiyo ya kupeleka Watanzania kupata uzoefu kwa migodi ya nje ya nchi.

Kiruswa alisema Serikali inajivunia uwekezaji wa ubia wa Barrick na matunda yake yanaonekana wazi.

"Ni hatua nzuri sana kwa Watanzania, hii itasaidia sana kuwa na wataalamu wengi katika sekta ya madini, nawapongeza sana Barrick kwa hatua hii nzuri," alisema.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri huyo ametoa agizo kwa migodi mingine yenye ubia na Serikali kuweka utaratibu wa kutoa ripoti ya utendaji kwa wananchi kupitia mikutano ya pamoja kama wanavyofanya Barrick.

'Kampuni zingine natoa maagizo waandae utaratibu kama huu wa kutoa ripoti zao kila baada ya robo mwaka, hii itasaidia kuona ni namna gani utendaji unafanyika na wananchi waone mafanikio yake," alisema Dk Kiruswa.

Katika ripoti yao, Barrick imeeleza imetumia dola milioni 14.1 (Zaidi ya Sh. Bilioni 35) kwa ajili ya kuwekeza kwenye miradi ya maendeleo.



# Wazazi kukamatwa kwa kukaidi kupeleka watoto shule

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

VIONGOZI wa halmashauri mkoani Singida wameagizwa kuwakamata na kuwafikisha mahakamani wazazi na walezi ambao wamekaidi kuwapeleka shule watoto wenye sifa ya kuanza darasa la kwanza na waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwanzoni mwa mwaka huu.

Agizo hilo lilitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba kwa nyakati tofauti wakati akizungumza na wakazi wa vijiji vya Kisonga, Mkulu, Mgongo, Mseko, Kizozo, Mgela na Mtoa wilayani hapa ikiwa ni ziara yake ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika halmashauri hizo.

Serukamba alisema ni lazima kila mtoto mwenyewe sifa ya kuanza darasa la kwanza na waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza kuanza masomo mara moja.

Alisema endapo mzazi au mlezi ataonekana kuwa kikwazo cha mtoto kuanza shule ni lazima achukuliwe hatua kali, ikiwa ni pamoja na kukamatwa na kufikishwa mahakamani kujibu mashtaka.

Serukamba, alisema kutokuwapeleka watoto shule ni kuwanyima haki yao ya msingi ya kupata elimu wakati huu ambao serikali imeboresha miundombinu ya elimu na kutoa elimu bure..

Aliwahimiza wananchi kuendelea kutumia msimu huu kuongeza juhudi zaidi katika kilimo na kuzalisha mazao mengi ya chakula na biashara kwa kutumia mvua zinazoendelea kunyesha nchini.

Serukamba aliwakumbusha wakulima kutumia mbegu bora na mbolea ili kuongeza uzalishaji wa mazao hayo.

Baadhi ya wakazi wa Kizonzo, walisema kijiji hicho kinakabiliwa na kero mbalimbali ikiwemo ukosefu wa maji safi na salama, hali inayowalazimu wanawake na watoto kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo. Vilevile, waliiomba Serikali kuwajengea zahanati na kuwaondolea adha ya kutembea umbali mrefu kwenda kufuata matibabu na wajawazito kujifungulia njiani.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent (kulia) akifuatiwa na Mkurugenzi wa Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), Samuel Mshote (katikati) na Mwakilishi wa Mkurugenzi Taasisi ya Utafiti wa Madini Tanzania (GST), Dk. Leonard Massawe, wakifuatilia wasilisho wakati wa kikao kuhusu mkakati wa kuzalisha mbolea kwa kutumia rasilimali zinazopatikana nchini, jijini Dodoma juzi. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Wekeza ya TIC yazidi kuchanja mbuga nchini

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMPENI ya Wekeza Tanzania inayoendeshwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) imefikia takribani mikoa 13 nchini kwa lengo la kutoa elimu kwa wananchi kuhusu uwekezaji na fursa zake zilizopo nchini.

Akizungumza wakati wa kufungua semina jijini hapa, Mkurugenzi wa Utawala na Msimamizi wa Rasilimali Watu, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Benjamin Chilumba alisema kuwa kupitia kampeni hiyo, wawekezaji na wafanyabiashara wa Mkoa wa Dodoma wamepata elimu kuhusu kusajili miradi, faida za kusajili na vivutio vinavyotolewa.

Chilumba, alisema serikali kupitia TIC serikali imeshusha kiwango cha mtaji kutoka Dola za Marekani 100,000 hadi Dola 50,000 na kuhamasisha zaidi Watanzania kusajili miradi ya uwekezaji. "Maboresho haya ya Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 2022 yanalenga kumkwamua Mtanzania kiuchumi, hivyo nitoe wito kwa wananchi kutumia fursa hizi katika mikoa yetu ili kujiendeleza kiuchumi," alisema

Meneja Uhamasishaji Uwekezaji wa Ndani wa TIC, Felix John, alisema kampeni hiyo ina lengo la kutoa hamasa na elimu sahihi ya uwekezaji kwa Watanzania na kuondoa dhana ya kuwa mwekezaji ni yule anayetoka nchi za nje.

Alisema kiwango cha mtaji kwa Mtanzania anayetaka kusajili mradi kimeshushwa mara dufu na kwamba TIC imerahisisha utoaji huduma kwa wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi kupitia kituo cha huduma mahali pamoja na ofisi za kanda kwa lengo la kuwawezesha kunufaika na vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi.

Kwa mujibu wa Felix, mwaka 2023, TIC ilifanikiwa kusajili miradi 504 na kuvutia mitaji yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 5.6 na ajira takribani 230,000 miradi itakapokamilika.

Alisema zaidi ya asilimia 45 ya miradi hiyo ni ya Watanzania na kuongeza kuwa katika mikoa hiyo waliyoendesha kampeni hiyo, imebainika kuwepo kwa fursa za uwekezaji katika kila sekta na kwamba kituo hicho kiko tayari kuendelea kusajili miradi ya uwekezaji.

Mmoja wa wawekezaji, Jacqueline Mwenzegule ambaye ni Mkurugenzi wa Sheria Itracom Fertilizers Ltd, alisema moja ya vitu vilivyomfanya aelewe umuhimu wa kusajili mradi TIC ni msamaha wa ushuru wa forodha kwa rasilimali za mtaji hususani mitambo na mashine inayotumika.

# Mahakama yajivunia teknolojia kufungua kesi majumbani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MTENDAJI Mkuu wa Mahakama nchini, Profesa Elisante Ole Gabriel amesema wananchi wanaweza kufungua kesi wakiwa majumbani kutokana na muhimili huo kutumia teknolojia kuendesha mashauri.

Akizungumza jana alipotembelea mabanda katika Wiki ya Sheria inayoendelea kwenye Viwanja vya Nyerere jijini hapa, Profesa Elisante, alisema kwa sasa teknolojia imekua kwa kiwango kikubwa mahakamani.

Alisema teknolojia hiyo kwa sasa inatumika katika utoaji haki, hivyo wananchi wakifika katika mabanda hayo, wanapaswa kuuliza maswali yatakayowasaidia kupata msaada wa kisheria.

Kuhusu wiki hiyo, alisema uzinduzi rasmi utafanyika leo na kilele chake Februari Mosi, mwaka huu, mgeni rasmi atakuwa Rais Samia Suluhu Hassan.

"Tunajivunia mahakama inakwenda na teknolojia katika utendaji kazi wa kila siku, hivyo hakuna ucheleweshwaji wa kesi zinazowasilishwa mahakamani," alisema.

Prof. Elisante, alisema wanaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu uendeshaji wa mahakama na kuwaomba kutumia maonyesho hayo kujifunza namna ya kutafuta haki kisheria.

Alisema katika wiki hiyo, jamii itapata msaada wa sheria na elimu.

# 'Walimu wahimizeni wanafunzi kutumia maktaba'

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule amewataka walimu wa shule za sekondari mkoani hapa kuwahimiza wanafunzi kutumia maktaba kujisomea na kupata matokeo mazuri katika mitihani yao.

Akizindua jana maktaba ya kujisomea ya wanafunzi iliyojengwa na Taasisi ya Genesis for Children Organization katika Shule ya Sekondari ya Mnadani jijini hapa, alisema kuwa maktaba zinatakiwa kuwa chachu kwa wanafunzi kujisomea kwa bidii na kuongeza maarifa kwenye masomo yao.

"Serikali ina kila sababu ya kuwashukuru wadau wa elimu ikiwemo taasisi hii ya Genesis ambayo imeona kusaidia moja ya shule zetu za sekondari 250 mkoani hapa," alisema na kufafanua kuwa:

" Kati ya hizo 42 zipo jijini na ni tisa tu zina maktaba kwa ajili ya wanafunzi kujisomea na kujifunzia."

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, alisema maktaba hiyo itasaidia wanafunzi kufanya rejea ya vitabu vya ziada na kiada na kuwajengea uwezo.

Awali akisoma risala kwenye uzinduzi huo wa maktaba shuleni hapo, Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Irene Kitoti, alisema ni ya pili kujengwa kwa Tanzania Bara kwa gharama ya Shilingi milioni 18.9 .

Irene, alisema kuwepo kwa maktaba hiyo ni matumaini yake kwa wanafunzi wa shule hiyo kutimiza ndoto zao za kupata elimu bora.





# COSOZA yatakiwa kulinda haki za wabunifu

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WASANII na wabunifu wametakiwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili Hakimiliki Zanzibar (COSOZA) ili kulinda maslahi yao na kupata haki zao.

Wito huo ulitolewa jana na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii ya Baraza la Wawakilishi, Hussein Ibrahim Makungu wakati wa ziara yake katika Ofisi za COSOZA zilizopo Mazizini Wilaya ya Mjini Unguja.

Makungu, alisema wasanii wengi hawafahamu haki na maslahi yao, hivyo ushiriki wao katika kupata elimu utasaidia

kulinda kazi zao kwa kutumia ofisi hiyo.

Alisema kwa mujibu wa sheria ni kosa kuiba kazi ya mbunifu au msanii bila ya makubaliano, hivyo ni vema kazi zao kulindwa na kuheshimiwa.

Kamati hiyo, haikuridhishwa na mazingira ya ofisi hiyo ambapo Makamu Mwenyekiti huyo alitaka Serikali kutatua changamoto hiyo ili watendaji waweze kufanyakazi zao kwa ufanisi zaidi.

Msimamizi wa ofisi hiyo, Mtumwa Khatib Ameir alisema kabla ya kuhamishiwa kwenye jengo la Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, walikuwa Wizara ya Katiba na Sheria.

Alisema katika jengo hilo, wanaendelea na majukumu yao vizuri ili kuhakikisha kazi za wasanii na wabunifu zinalindwa.

Mkurugenzi Idara ya Leseni, Ukaguzi na Mirabaha, Muumini Mwinyi Mzee, alisema ofisi yao imekuwa ikifanyakazi na mataifa mbalimbali duniani kuhakikisha haki za wasanii na wabunifu Zanzibar zinazingatiwa.

Kamati hiyo yenye wajumbe 12 imefanya ziara katika Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda na kutembeleza idara na ofisi zote zilizopo chini ya wizara hiyo kufuatilia utendaji kazi.

# 'Acheni kutoa lugha za matusi'

**Na Rahma Suleiman**
ZANZIBAR

MFUKO wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF) umewataka wanachama wake kufuata sheria na kuacha kutoa lugha za matusi kwa watoa huduma katika vituo vya afya na hospitali visiwani hapa.

Rai hiyo ilitolewa jana na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa ZHSF, Yaasin Ameir Juma wakati akitoa elimu ya mfuko huo kwa wafanyakazi wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto katika Wilaya ya Mjini visiwani hapa.

Juma alisema kuwa kuna wanachama wanatoa lugha hizo na kuwafokea watoa huduma huku wakiwalazimisha wawape rufaa ya kwenda kwenye hospitali wanazotaka kupata huduma za afya kinyume na sheria.

Alisema ili mgonjwa apate rufaa lazima kuwe na uthibitisho kutoka kwa daktari kwa kesi maalum.

Alionya kuwa mwanachama atakayechukua rufaa bila maelekezo ya daktari, Serikali haitahusika na gharama zozote.

"Kama watu wote watamiminika katika Hospitali ya Rufaa Mnazi Mmoja kutafurika na kusababisha madaktari kuzidiwa na kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi," alisema Juma.

Aliwataka wanachama hao kuwa na busara na madakatri kufanya kazi kwa mujibu wa taratibu na sheria za mfuko huo.

"Hebu tutizame jamani daktari ukimtolea maneno machafu ataweza kufanya kazi kwa moyo mkunjufu na kukupa huduma nzuri kama inavyostahili, tubadilikeni wenzangu,"

Ofisa Uhusiano wa ZHSF, Asha Kassim Biwi aliwataka wanachama hao kujenga imani na mfuko huo ili kutoa huduma bora za afya kwa wote.

Kwa upande wao, wafanyakazi hao wameomba uongozi wa ZHSF kutoa elimu zaidi kwa wanachama ili kufikia malengo yaliokusudiwa na Serikali.

Walisema elimu hiyo itawasaidia kuondoa usumbufu wa kupata rufaa na huduma katika vituo vya afya na hospitali visiwani hapa.




Meneja wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi, Magonjwa ya ngono na Homa ya Ini (NASHCOP) wa Wizara ya Afya, Dk. Anath Rwebembera (katikati), akizungumza wakati wa kufungua mkutano wa mazungumzo kati ya shirika la Amref na wizara hiyo, jijini Dodoma jana, Kushoto ni Mkurungenzi wa mradi wa afya thabiti shirika la Amref, Dk. Edwin Kilimba na Naibu Meneja wa Mpango wa Taifa wa Kifua Kikuu na Ukoma, Dk. Liberale Mleoh. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waandishi vijana wapewa changamoto

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania Zanzibar (TAMWA Zanzibar), Dk. Mzuri Issa amewataka waandishi wa habari vijana kuongeza juhudi kuandika habari za wanawake na uongozi ili kuishawishi jamii kuwaunga mkono kuelekea Uchaguzi Mkuu utakaofanyika nchini mwakani.

Akizungumza jana katika mkutano uliowashirikisha wadau kutoka Shirika la National Endowment for Democracy (NED), waandishi wa habari vijana, wakurugenzi wa redio na wahariri wa vyombo vya habari, Dk Mzuri, alisema kuna mambo yanawakwaza wanawake kugombea uongozi katika chaguzi mbalimbali nchini.

Alisema TAMWA kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wamekuwa wakitoa mafunzo kwa waandishi wa habari ili kuwaongezea ujuzi wa kuandika habari za wanawake na uongozi na kuondoa mitazamo hasi katika jamii.

"Tunaelekea kipindi cha Uchaguzi Mkuu 2025, waandishi wa habari tunawategemea katika upande huu kuandika zaidi na kufanya vipindi vingi ili tuone kasi ya wanawake inakuwa kubwa kugombea ngazi mbalimbali majimboni," Dk Mzuri.

Meneja wa Mradi wa YMF Afrika, Merry Kangunyi alisema kuwa wamefarijika na jitihada zinazofanywa na TAMWA Zanzibar kushawishi jamii kuondokana na mitazamo hasi, husan wanawake kugombea uongozi.

"Tumefarijika na kazi kubwa inayofanywa na TAMWA Zanzibar kuongeza nguvu na kuifahamisha jamii kujua haki zao na kugombea nafasi za uongozi kuanzia ngazi ya familia hadi Taifa," alisema Merry.

Ofisa mradi huo kutoka TAMWA, Tatu Ali Mtumwa, alisema waandishi wa habari ni chachu ya maendeleo kwa kuhamasisha usawa wa kijinsia ili kufikia asilimia 50 kwa 50 kwa wanawake na wanaume katika ngazi za maamuzi.



**ZARI**

UKURASA 13

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI





# SASA IMEHITIMISHWA

LIKUWA majigambo na kutishiana baina ya mastaa wawili nchini Haji Manara na Dulla Makabila, wote wawili wakipigania kwa nguvu zote penzi la mrembo Zaylisa.

Makabila ambaye alikuwa mume wa Zaylisa na Haji ambaye kwa sasa yupo katika penzi zito na mrembo huyo kwa wiki kadhaa wamekuwa katika malumbano makali katika mitandao ya kijamii.

Hata hivyo, Haji ameibuka mshindi wa pambano hilo baada ya kuamua kufunga ndoa na mrembo huyo na kumfunga mdomo mwanamuziki huyo wa singeli.Ushindi huo haukuja hivi hivi, bali ilimbidi kutumia nguvu nyingi na mbinu za medani hadi kufanikisha lengo lake ambalo lilitishiwa kufutika.

Kilichotokea ni kwamba wakati Haji na Zaylisa wakifunga ndoa ya kimyakimya, Dulla Makabila kwa upande wake alikuwa akihangaika kutii wito wa kituo cha polisi cha Oysterbay ambao ulimtaka kuripoti hapo kwa kile kinachodaiwa matumizi mabaya ya mtandao.

Haijafahamika kama kufungwa kwa ndoa hiyo itakuwa hitimisho la mpambano huo ambao uliwagawa watu kutokana na mitizamo yao tofauti na wengi wakimlaumu Makabila kwa kushindwa kukubali kama ameachwa.

BASI SAWA

## Irene Uwoya kawa mchungaji



Tangazo la mwigizaji mkongwe wa Bongo Muvi, Irene Uwoya, kuwa ameitikia wito wa Mungu na kuwa mchungaji, limeonekana kupokelewa tofauti na wafuasi wake.

Muigizaji huyo ambaye amekuwa kivutio kutokana na maisha yake ya anasa, anatarajia kuanzisha kanisa lake ambalo yeye atakuwa mchungaji wake.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, idadi kubwa wafuasi wake walitoa pongezi kupitia chapisho lake lenye nembo ya jina linalokisiwa kuwa ni la kanisa lake, wakieleza ni mwanzo mzuri kwa msanii huyo ambaye ni mama wa mtoto mmoja.

## Akothee aonyesha huruma

MWANAMUZIKI kutoka Kenya, Esther Akoth, maarufu kama Akothee amemchukua mtoto mmoja wa kiume anayesoma shule ya msingi kutokana na kuishi katika mazingira magumu.

Mtoto huyo amekuwa na maisha magumu baada ya mama yake mzazi ambaye anaishi naye kuwa na matatizo ya kiakili.

Msanii huyo mwenye watoto watano aliweka video kwenye akaunti yake ya Instagram ikimuonyesha mtoto huyo aliyetambuliwa kwa jina la Samson akimuandaa kwa ajili ya kwenda shule.





# VANILLAH AZIDI KUPAA

MWANAMUZIKI kutoka lebo ya Kings Music, Vanillah, amekuwa gumzo kupitia wimbo wake mpya 'Sijazoea' na kutajwa kama mrithi wa Ali Kiba.

Kutokana na sauti yake nzuri na yenye hisia, imefanya ngoma hiyo kufanya vizuri katika mtandao wa YouTube kwa kutazamwa na watu wengi kuliko wimbo wowote uliotambulishwa mwezi huu.

Baadhi ya wadau wa muziki wamesema Vanillah anakidhi vigezo vingi vya kuwa mwanamuziki bora na hivyo kumtaka Ali Kiba kuzidi kumtengeneza bila kuchoka.



# Zari awapa neno wambea wa mitandaoni

MFANYABIASHARA na mwanamtandao maarufu, Zari maarufu kama The Boss lady, amesema wanawake wengi hawatumii mitandao ya kijamii kujiinua kiuchumi na badala yake wanatafuta umbea.

Akizungumza hivi karibuni, Zari amesema kwa upande wake amefanikiwa kutokana na matumizi bora ya mtandao kwa kutangaza biashara zake.

"Nimekuwa na nidhamu katika kutumia mitandao, nimekuwa nikipanga muda wangu wa kazi ,kukaa na watoto na kuperuzi kwenye simu. Wanawake wengi wanatumia kwa ajili ya umbea na kupiga soga badala ya kutafuta pesa,"amesema.

# DULLA MAKABILA HAYUPO PEKE YAKE

**Adam Fungamwango**

ILIKUWA wiki ngumu mno na yenye pilikapilika nyingi. Mitandao ya kijamii ilichafuka.

Bifu likawa kubwa, wasomaji wa mitandao ya kijamii wakagawanyika sehemu mbili.

Hii yote ni baada ya msanii wa muziki wa singeli kutoka ngoma yake mpya kwa mtindo wa audio, iitwayo 'Furahi.'

Ngoma hii iliachiwa Januari 19, lakini ikiwa na wiki moja na siku moja sasa ndiyo inashika namba moja kwa 'kutrendi' kwenye mtandao ya 'you tube.'

Kwa walioisikiliza, inasemekana baadhi ya maneno yamemlenga mtalaka wake, Zaylisa.

Dhana hii haitakuwa ya kwanza kwa wasanii kuimbana, au kuwaimba wake au wapenzi baada ya kukorofishana na kuachana nao.

Ilianza miaka mingi nyuma, hivyo kama ni kweli Dulla Makabila hayupo peke yake, hatokuwa wa kwanza wala wa mwisho.

### Juma Nature-Inaniuma Sana

Nature aliachia wimbo huu mwaka 2002 ambao ulitingisha mno kwenye tasnia ya muziki wa bongo fleva ambao ulikuwa unajijenga kipindi hicho.

Ngoma hiyo ilikuwa kwenye albamu ya 'Ugali' na hakuna yeyote ambaye hakuambiwa au alikuwa akimuimba aliyekuwa mpenzi wake kipindi hicho, msanii wa filamu, Sinta.

Hiyo ndiyo dhana iliyojengwa na kuaminika wakati huo. Kama ni kweli au la, lakini habari ilikuwa hivyo.

### Nuhu Mziwanda-Jike Shupa

Msanii huyu wa bongo fleva, 2016 alifyatua ngoma moja matata sana iliyopendwa na mashabiki wengi akimshirikisha Ali Kiba, akaiita 'Jike Shupa.'

Hata hivyo, wengi wa mashabiki walioisikiliza ngoma hiyo walidai alimuimbia aliyekuwa mpenzi wake, msanii wa bongo fleva, Shilole.

Na hii iliaminika zaidi kwa sababu hata aliyecheza kama 'video queen' alifanana naye sana, na wimbo huo ukampa chati na kumfanya msanii huyo kuwa staa hadi leo hii, na yeye akajipachika jina la Jike Shupa.

### Lady Jaydee-Mambo Matano

Hii ni moja kati ya ngoma 10 bora ya kumalizia mwaka 2023 kama ilivyochaguliwa na mashabiki wa muziki na wasomaji wa gazeti hili.

Wimbo huu kwa mashabiki wanaosikiliza wanadai ni dongo kwa mpenzi wake wa zamani walieachana naye, Spicy ambaye naye ni msanii wa Kinigeria.

### Juma Nature-Sitaki Demu

Inavyoonekana Juma Nature aliumia sana, baada ya ngoma 'Inaniuma Sana' akaja na ngoma nyingine akaiita 'Sitaki Demu.' Wajuzi wa mambo wakasema wimbo huo nao aliimbwa yule yule,'Sinta.'

### Harmonize-Single Again

Machi 27 mwaka jana, msanii Harmonize alipandisha ngoma aliyoiita 'Single Again'. Na hii ni wiki kadhaa baada ya kuachana na mpenzi wake, msanii wa filamu, Kajala Masanja.

Na hiyo ilikuwa ni mara ya pili kwa wapenzi hao kuachana. Waliachana awali, wakarudiana. Wakaachana tena. Jamaa akatoa ngoma hiyo.



FILAMU

# Msuto Daily: Umbea utakukondesha

**Na Adam Fungamwango**

MAZOEA siku zote yana tabu. Haijalishi umezoea tabu au raha. Wapo watu ambao wamezoea kukaa kijijini, wanapofika mijini na kukaa wiki moja tu hamu inawaishia wanataka kurudi walikotoka. Ni kwa sababu ya mazoea.

Kuna wanaotoka mjini kwenda kijijini, nao wanapokutana na mazingira ya huko, yanawashida kutokana na kuzoea kuishi mjini, hivyo wanashindwa.

Hata leo hii mkazi wa 'uswazi', anaweza kushindwa kukaa 'ushuani.'

Tunaitazama filamu ya 'Watoto wa Mitaani', imechezwa na wasanii wengi chipukizi, lakini wakiongozwa na Ben Blanco. Wengine ni Salma Juma, Peter Phimar, Kisegese, Kadogo, Dulla Said, Dogo Mandal, Julius Fred na wengineo wengi.

Baada ya kupata kibali kutoka serikalini, Blanco anaanza kazi ya kukusanya watoto mitaani kwa ajili ya kituo cha watoto yatima.

Haikuwa kazi rahisi. Ben Blanco alikumbana na changamoto nyingi kutoka kwa watoto hao kuanzia wa miaka mitatu hadi 17, ambao wengi walikuwa wameshazoea maisha ya kuzurura, kulala jalalani na kula chochote kinachopatikana. Ni maisha ambayo wamezoea, hivyo kwenda kukaa kwenye kituo ilikuwa mtihani mkubwa.

Waliopatikana maisha yao walianza kubadilika. Walianza kuwa wasafi kwa sababu ya kuoga mara kwa mara. Siha yao ilianza kubadilika, kwani walianza kunawiri. Ni kwa sababu walianza kula wanachokitaka na si wanachokipata. Pia walianza kusomeshwa. Hata hivyo bado baadhi ya watoto waliona hiyo ni kama kunyimwa uhuru wao. Walizoea kurura kutwa nzima wakitafuta wasichokijua wala kuwa na uhakika wa kukipata. Lakini walizoea maisha hayo, hivyo maisha ya kuchungwa, kukaa kutwa nzima wakisoma tu, wakila, kunywa kiulaini, kufanya kazi mbalimbali za kituo, waliona kama ni aina fulani ya utumwa.

Wengine walianzisha kampeni ya kutoroka ili wakaendelee na maisha yao ya zamani yaliyokuwa kama ndege. Walifanikiwa baada ya kumfungia msalani, watoto wakakimbia na kumuacha binti mwenye miaka mitatu, Kadogo ambaye alisalia na Blanco aliyekuwa akiwalea na kuwahudumia.

Maisha yao ya mara ya pili mitaani hayakuwa mazuri. Ni kwa sababu tayari walishaonja aina fulani ya maisha ya kuhudumiwa, kula wanachokitaka na hawazururi kusaka chakula.

Walianza kukonda. Kitendo cha kurejea tena mitaani, walipoteza muonekano wao na kuwa machokoraa yalioweza hata kutazamika.

Wote kwa ujumla waligundua makosa yao, wakajikusanya na kwenda kuomba radhi kwa Blanco wakiomba kurudishwa kituoni. Walikubaliwa na kuanza maisha mapya.





# Phyna wewe unamfuata mume au....

ALIYEKUWA mshiriki wa shindano la Big Brother Naija, Phyna amesema kuwa hawezi kuchumbiana na mwanaume aliyezaa mtoto ili kuepuka vituko vya mwanamke aliyezaa naye.

Phyna amesema kwamba mwanaume ambaye awali alikuwa na mke na kuzaa naye watoto na kisha kuachana, huwa ni tabu kwake kuingia katika uhusiano naye wa kimapenzi kwa sababu atakuwa na majukumu katika sehemu mbili.

Phyna amesema kuchumbiana na mwanaume wa aina hiyo itakupa matatizo kutokana na mama watoto wake kufanya vituko ambavyo kamwe huwezi kuvumilia.



## Ukali wa Baba Spyro usipime

MWIMBAJI nyota kutoka Nigeria, Spyro amesema kutokana na ukali wa baba yake ambaye ni mchungaji ulisababisha kuchukia dini.

Akizungumzia maisha yake ya utotoni, Spyro kama mtoto wa mchungaji, alikulia katika maisha ya amri kali na taratibu za kufuatiliwa kiasi ambacho aliamini suala la dini kama chukizo kwake.

"Baba yangu alikuwa mkali sana, yeye ni mchungaji kwa hiyo unajua wachungaji wanavyokuwa na watoto wao. Kwa kweli ni wakali kwa sababu wana itikadi hii kwamba watoto wao ndio kama warithi.

Shinikizo sio nzuri, lazima niseme. Lakini sikumjua Mungu kupitia baba yangu, ingawa nilikuwa mbele ya Biblia," amesema.

## Tiwa Savage aibiwa akiwa London

MWANAMUZIKI na mtunzi wa nyimbo, Tiwa Savage amesema ameibiwa mali zake wakati akikatiza katika jiji la London nchini Uingereza.

Katika tukio hilo lililotokea mwishoni mwa wiki hii, mwimbaji huyo amesema alikabiliana na wezi ambao walimpora vitu vyake na kumfanya kuwa na wasiwasi kuhusu usalama wake.

"Jamani jiji la London limenifanya kuwa na hofu, nimeibiwa jana," ameandika Savage kupitia ukurasa wake wa Instagram.





## Edochie awaaga mashabiki baada kuteuliwa waziri

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Yul Edochie, ambaye ameteuliwa kuwa Waziri, amewaambia mashabiki zake kwamba kazi yake hiyo haitamfanya kuacha kucheza filamu, badala yake atapumzika kwa muda.

Akijibu swali kutoka kwa mashabiki zake kupitia ukurasa wake wa Instagram, Edochie amesema katika safari yake hiyo mpya akiwa kama waziri ni kama kutimiza wito wake, na sio kuua kipaji chake.

"Mamilioni ya mashabiki wangu bado wanataka kuniona nikiigiza kwenye filamu, msiwe na wasiwasi watu wangu, siendi kabisa. Lazima nitimize hatima yangu. Kazi ya Mungu ndiyo hatima yangu. Na kazi ya Mungu lazima ifanyike," amesema.

## 21 Savage awakubali wazazi masikini

RAPA mkali kutoka Marekani, 21 Savage amesema bora kuwa na wazazi masikini kuliko matajiri kwa sababu utaishi maisha yenye furaha na uangalizi wa muda mrefu.

"Kwa mtazamo wangu naamini wazazi masikini ni bora zaidi ya matajiri. Mzazi ambaye hana kipato anapata muda mwingi kukaa na watoto, mwenye kipato anaweza kununua zawadi ingawa sio muda wote.Watoto wanapenda kutumia muda mwingi wakiwa na wazazi na muda hauna gharama yoyote" - amesema 21 Savage

21 Savage amefunguka hayo kupitia mahojiano aliyofanya na Shannon Sharpe,, baada ya kuulizwa kuhusu maisha yake, uhusiano na kazi za muziki.







# Miti 200 yapandwa Arumeru

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

ZAIDI ya miti 200 ya jamii ya Acasia imepandwa katika maeneo ya Shule ya Sekondari Losinoni Wilaya ya Arumeru mkoani hapa ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira kutokana na kilimo cha bangi.

Miti hiyo imepandwa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) Kanda ya Kaskazini , Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Wakala wa Misitu nchini (TFS) wilayani Arumeru, Asasi ya Kimara Peer Educators, viongozi wa dini na Kijiji cha Losinoni ilipo sekondari hiyo.

Akizungumza jana wilayani Arumeru wakati wa upandaji miti hiyo katika maeneo ya sekondari hiyo, Ofisa Elimu Jamii wa DCEA Kaskazini, Shabani Miraji, alisema ni kuelekea kusheherekea siku ya kuzaliwa mwanamazingira namba moja nchini, Rais Samia Hassan Suluhu Januari 27, mwaka huu.

Miraji alisema kuwa wamepanda miti hiyo kwa sababu ni stahimilivu kwa mazingira ya eneo la kijiji hicho.

Alisema vilevile wameamua kupanda miti hiyo baada ya kubaini miti mingi imekatwa kutokana na kilimo cha bangi.

"Kilimo cha bangi husababisha ukataji hovyo wa miti na uharibifu wa mazingira. Hivyo zoezi la kupanda miti litasaidia kutunza mazingira yaliyoathiriwa na zao hilo haramu," alisema.

Alisema kampeni hiyo itahamasisha jamii kuachana na kilimo cha bangi ili kunusuru mazingira na kuanza kupanda miti ya matunda, kivuli na mazao ya chakula, kama vile maharage, mahindi na karoti.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mwandamizi wa DCEA wa Kanda hiyo, Sarah Ndaba, alisema wameamua kuanza na wanafunzi kwa sababu tafiti zinaonyesha bangi ni miongoni mwa dawa za kulevya za awali ambazo vijana wa umri mdogo wanaanza kutumia kabla ya kuhamia dawa nyingine. "Wanafunzi hawa ndio mabalozi wa kufikisha elimu hii majumbani kwa wazazi wao, ambao ndo walikuwa wakulima wakubwa wa zao hili.

Tangu elimu ilipoanza kutolewa na DCEA Kaskazini, imeleta mabadiliko makubwa kwa wakulima wa eneo hilo kwa kuachana na kilimo cha bangi na kujikita kwenye mazao ya chakula ya yakiwemo mahindi, maharage na karoti. Kilele cha siku hiyo kitafanyika yalipotokea maporomoko ya mawe na matope Katesh wilayani Hanang Mkoa wa Manyara mwishoni mwa mwaka jana na kuua watu kadhaa, kujeruhiwa na nyumba kubomoka

# Baba adaiwa kumchinja mwanawe kichwa, kiwiliwili vyakutwa kwenye ndoo

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Arusha linamshikilia mwendesha bodaboda, Amedius Mfoyi (25), Mkazi wa Muriet kwa tuhuma za kumchinja mwanawe mwenye umri wa miaka mitatu na kutenganisha kichwa na kiwiliwili.

Mtoto anayedaiwa kuuawa kikatili, Amani Amedius Mfoi mwili wake umekutwa umehifadhiwa kwenye ndoo mbili tofauti.

Baadhi ya majirani wa mtuhumiwa huyo, wanahusisha mauaji hayo na imani za kishirikina kutokana na kudai amekuwa akisimulia mara kadhaa anavyotamani kuwa na utajiri wa kufuru katika uhai wake.

Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Arusha, Justine Masejo amethibitisha mtuhumiwa huyo kumuua mtoto wake huyo Januari 23, mwaka huu majira ya jioni katika Mtaa wa Murieti, Tarafa ya Elerai jijini Arusha.

Kamanda Masejo alisema kuwa mtuhumiwa huyo alimuua mtoto wake huyo kwa kumchinja kwa kitu chenye ncha kali kisha kutenganisha kichwa na kiwiliwili.

Alisema baada ya polisi kupata taarifa za mauaji hayo, kwa kushirikiana na wananchi walianza kufanya uchunguzi na kumsaka mtuhumiwa huyo na kufanikiwa kumkamata.

Alisema baada ya uchunguzi wa mauaji hayo kukamilika, jalada la mauaji hayo, litapelekwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS) kwa hatua zaidi za kisheria dhidi ya mtuhumiwa huyo.

Akizungumza jana kwa masikitiko, babu wa marehemu ambaye pia ni mjumbe wa nyumba 10, Isack Mfoyi, alisema nyumbani kwake anaishi na mjukuu wake na mke wake.

Mfoyi, alisema siku ya tukio hilo alilala na mjukuu wake na kulipokucha mkewe alisafiri kwenda Moshi mkoani Kilimanjaro, na yeye na Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa kwenye majukumu ya jamii.

"Nikarudi mchana kwenye saa nane, lakini hapa nyumbani nilimuacha mjukuu wangu na baba yake, nilimuuliza mwanangu mjukuu wangu yupo wapi, akanijibu amelala na muda huo huyu mwanangu alikuwa anadeki chumba chake nikajua anafanya usafi wa kawaida," alisema.

Alisema wakati akiendelea na shughuli zake za ujasiriamali nje ya nyumba yake, alipatwa na wasiwasi baada ya kuona muda unazidi kwenda bila kumuona mjukuu wake.

"Nilirudi tena kumuuliza mtoto yupo wapi na hivi sasa ni jioni sijamuona, amelala muda wote huo, akajibu sijui nikaingia ndani nikiwa nimemuacha nje amejiinamia kichwa chini," alisema na kuongeza kuwa:

" Kabla sijaingia ndani nikamwambia nenda katoe taarifa Polisi kuwa mtoto wangu (wake) ametoweka simuoni.

Nikaingia ndani, majira ya saa 12:00 jioni nikasikia harufu ya makande kuungua, nikaenda kuchukua maji niongeze, kufunua ndoo nikakuta kichwa cha mjukuu wangu, nikashtuka ikabidi nifunue ndoo nyingine, nikakuta kiwiliwili."

Alisema wakati akitoa taarifa kwa majirani, mwanawe huyo alikuwa hayupo nyumbani baada ya kutoweka na kwenda kusikojulikana.

Alisema wakati wanajindaa na majirani hao kwenda kituo cha polisi kutoa taarifa kuhusiana na mauaji hayo, alipita askari anafahamiana naye na kumweleza mkasa huo.



Ofisa miradi wa shirika lisilo la kiserikali la Haki Madini, Emmanuel Mbise (kulia), akizungumza kwenye mafunzo ya kuwajengea uwezo wanawake wachimbaji madini ya Tanzanite, madalali na wajasiriamali, katika Mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Waziri awashukia TANESCO katakata umeme mipakani

**Na Hamida Kamchalla,**
MKINGA

SHIRIKA la Umeme nchini (TANESCO) limetakiwa kuacha kutoa mgao wa umeme katika maeneo yenye vyanzo vikubwa vya mapato ya mipakani kwa sababu linaikosesha serikali kiwango kikubwa cha mapato kutoka nchi jirani.

Wito huo umetolewa na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Dastan Kitandula wakati wa kuwasha umeme wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) katika vijiji vya Magodi na Kigandini Kata ya Kasera wilayani hapa Mkoa wa Tanga.

Kitandula alisema mgao wa umeme umekuwa ukiathiri kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa mapato ya Serikali katika mpaka wa Horohoro wilayani hapa kutokana na TANESCO kukata nishati hiyo mara kwa mara kila siku.

Alisema Serikali inafanya jitihada kubwa kuhakikisha umeme unapatikana kwa sababu mahitaji yaliyopo ni makubwa ikilinganishwa na unaozalishwa na shirika hilo na kupelekea baadhi ya maeneo nchini kupata mchache.

" Wilaya ya Mkinga hali ni ngumu kila siku iendayo kwa Mungu umeme lazima ukatike, tunaelewa wenzetu wanaangalia kile kidogo wanakipeleka maeneo ya uzalishaji ili kusikosekane mapato ya serikali, Mkinga hatuna viwanda, kwa hiyo ni rahisi sana TANESCO kutuweka pembeni," alisema na kuongeza kuwa:

"Wanasahau jambo moja kubwa, Mkinga tuna kiwanda kikubwa kinachotuingizia mapato, ambacho ni ule mpaka (Tanzania na Kenya), ile mizigo inayopita pale inatuingizia mapato makubwa sana, lakini wenzetu wanajisahau pale panahitaji umeme muda wote."

Naibu Waziri huyo alisema mgao huo wa umeme unaathiri kwa kiwango kikubwa kituo chao kwa kukosa umeme na mapato ya Serikali.

" Wakati mwingine kwenye kituo cha pamoja, Wakenya wanatoka na kulazimika kurudi upande wao ili waweze kufanya kazi sasa niombe, umeme kwa upande huu wa Mkinga usikatwe kwa sababu tunapoteza mapato," alisema.

Aliitaja kero nyingine sugu iliyopo katika Wilaya ya Mkinga kuwa ni ukosefu wa maji ambayo imedumu kwa miaka mingi.

Hata hivyo, aliishukuru serikali kwa ujenzi wa mradi mkubwa wa maji unaotekelezwa katika wilaya hiyo. "Tunaishukuru serikali kwa kutuletea mradi mkubwa wa maji kutoka Mto Zigi hadi Horohoro wenye thamani zaidi ya Shilingi bilioni 35, tunaomba Mkandarasi yule aendelee kumsimamia kazi ile ikamilike kwa wakati," alisema.

Akizindua kuwashwa kwa umeme huo, Naibu Waziri Mkuu, Dk. Dotto Biteko alisisitiza kuwa kero zote zinazowakabili wananchi zitafanyiwa kazi kabla Rais Samia Suluhu Hassan kupita kwenye maeneo yao.

Biteko ambaye pia ni Waziri wa Nishati, alisema haitakuwa vema kama kiongozi wa ngazi ya juu akipita kwenye maeneo hayo na kukutana na kero za wananchi.

Baadhi ya wakazi wa vijiji hivyo vya Magodi na Kigandini waliishukuru Serikali kwa kuwapelekea umeme na kuwanyamazisha kilio chao kikubwa cha muda mrefu.

"Kabla ya umeme kutufikia tulikuwa na kero nyingi, hospitali wakina mama walikuwa wanajifungua kwa shida, jenereta haikuwa ikikidhi mahitaji mpaka kusafiri kwenda Hospitali ya Wilaya Mkinga," alisema Mwajuma Omari.

Mwajuma, alisema kutokana na maeneo yao kupata umeme, wataanzisha viwanda vidogo na kuzalisha bidhaa, kuuza na kujiingizia kipato.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# ZUNGU LA UNGA BILLY DRAGO

## -Ndiye adui katili zaidi, dharau kuwahi kutokea

Na Adam Fungamwango

WAPO wanaomwita, Carlos. Wengine zungu la unga. Jina lake kamili ni William Eugene Burrows. Lakini mwenyewe akajipa jina la Billy Drago.

Anatajwa kuwa ni adui katili zaidi kuwahi kutokea kwenye filamu za ubabe, muuaji, fujo, utekaji na matukio yanayofanana na hayo.

Anakuua huku akikuchekea. Hajawahi kukasirika hata siku moja. Hasira zake ziko ndani ya moyo wake.

Anaweza kukata kipande kimoja baada ya kingine cha nyama ya adui yake akiwa hai, akawa anakula mbichi huku akimrimgishia na kucheka, akiwa kama hajafanya kitu chochote cha ajabu.

Sura yake, na muonekano wake ukimuona kwa mara ya kwanza huwezi kudhani kuwa ni mtu mmoja mwenye ukatili wa kupitiliza, ulioangukia kwenye unyama.

Anatajwa ni adui hatari zaidi kwa sababu wajihi wake na tabia yake ya upole, manjonjo, dharau, kebehi, kucheka na kutoonyesha hasira zake hadharani, hakuna aanayejua ni wakati gani anaweza kumuua adui yake, tofauti na wale wengine.

Anaweza kumchinja yoyote yule hata mfanyakazi au ndugu yake anapogundua kuna chembe chembe za usaliti ndani yake.

Huyu ndiyo Billy Drago, aliyezaliwa November 30, 1945 nchini Marekani na mauti yakamkuta June 24, 2019.

Wale watoto, vijana au watu wazima waliokuwa wakiangalia filamu miaka ya 1980, hadi 1990 kwenye vibanda umiza watamkumbuka sana mwamba huyu aliyecheza filamu nyingi lakini kwa kuwakumbusha tu baadhi ni The Delta Force namba mbili, 1990, Pale Rider 1985 ,Invasion USA 1985 Death Ring 1992 na nyingine nyingi sana ambazo baadhi alicheza na staa, Chuck Norris.

Asilimia zaidi ya 90 amecheza kama adui mkuu kwenye filamu zake. Amecheza zaidi ya filamu 100 katika uhai wake.

Kama nilivyotangulia kuandika kuwa hakuwa anatumia nguvu kubwa sana katika kutimiza majukumu yake kama adui, alikuwa mtu pia fulani hivi, hana kelele, mwili wake hauna misuli, hata uongeaji wake ulikuwa ni wa utaratibu sana.

Katika hali isiyo ya kwaida, hakujua hata kurusha teke wala ngumi, lakini alikuwa mmoja wa maadui katili na wa kuogopwa hata na waliokuwa wakiziangalia tu filamu zake za kikatili.

Maadui hata 10 wanaweza kumuwekea bastola kichwani badala ya kuogopa akacheka tu, halafu akawaambia bila wasiwasi,"kwa nini nyinyi ndiyo msishushe bastola zenu nikawateka mimi?"

Alijipatia heshima na umaarufu mkubwa kuanzia miaka ya 1980 kwani hakuna mpenda filamu yoyote wa miaka hiyo hadi mwanzoni mwa miaka ya 2000 asiyemfahamu.

Labda jina lake tu linaweza kukuchanganya, lakini siyo sura yake, ukiiona tu unaanza kukumbuka vimbwanga na ukatili wake.

Siku zote alicheza kama adui mkuu au kubwa la maadui, jambazi, kinara wa uuzaji wa madawa ya kulevya, magenge ya uhalifu, lakini pia akiwa na sifa ya ukatili mkubwa.

Labda kuna wanaojiuliza kama hakujua hata kurusha teke au ngumi anakuwaje katili au muuji?

Ni kwamba kutokana na kuwa yeye hucheza kama bosi wa wahalifu, au wauza madawa ya kulevya, basi huwa tajiri mwenye ukwasi mkubwa ya fedha na kwa maana hiyo huajiri watu mbalimbali wataalam wa mapigano ya aina mbalimbali, mabausa, wauaji wa aina mbalimbali waliokubuhu, majambazi na kila aina ya watu makatili mwenye uwezo wa kuua na kutesa ataajiriwa na yeye.

Na wengine watakuwa na kazi moja tu ya kumlinda, acha wale wanaolinda biashara zake haramu.



Kundi la Billy Drago.

Kwa hiyo yeye kazi yake inakuwa moja tu, kutesa, kuamrisha na kuua yoyote yule anayeona anakwamisha mipango yake, ikiwemo hata wale aliyowaajiri na anafanya hivyo akiwa analidwa na kikosi chake maalum.

Kumuua au kumteka yeye ni mpaka ukimalize kikosi chake hicho ambacho mara nyingi ilikuwa ngumu mno na mastelingi wengi waliipata freshi, ila ukifanikiwa jamaa anakuwa hana ujanja, ingawa alikuwa anajua sana kutumia bastola anayokuwa nayo mkononi muda wote.

Huyu jamaa unaweza kukamatwa na serikali, akawa hana hata wasiwasi na nyodo juu kuwa atakuja kukombolewa na kundi lake la magaidi, na kweli inakuwa hivyo.

Anaweza hata kutekwa kiongozi kwa nia ya kushinikiza bosi wao aachiwe huru, ikawa kama ilivyopangwa.

Ni mcheza filamu wa Kimarekani aliyekuja kubadilisha aina ya uchezaji wa maadui kwenye soka la picha na kupendwa mno kiasi cha kupewa kazi nyingi kucheza.

Ilizoeleka kuwa adui ni lazima uwe na nguvu, misuli mikubwa, sura ya kutisha, nzito, mbaya na mwenye hasira muda wote, hata wakati wa kutoa adhabu au kutoa amri, lakini kwake haikuwa hivyo, akaleta kitu kipya kwenye tasnia ya filamu ambayo ilipendwa na kukubalika kiasi cha kupata mikataba mingi, akicheza filamu zaidi ya 100.

Akiwa mdogo alianza kupenda kuwa mwigizaji kutokana na baba yake kupenda kumpeleka kwenye majumba ya sinema


Aliacha kazi ya Uandishi wa Habari na kucheza tamthilia kwenye vipande vya televisheni na filamu yake ya kwanza ilikuwa ni mwaka 1987 The Untouchables iliyobadilisha ukurasa wa maisha yake kiasi kwamba hadi anafariki 2019 akiwa na utajiri mkubwa.

**Tuma meseji 0716 350534**



Billy

## HABARI KIMATAIFA



# Rais Ruto apata pigo lingine

**NAIROBI,** KENYA

MAHAKAMA kuu nchini Kenya imezuia serikali kupeleka kikosi cha polisi Haiti na kutaja hatua hiyo ni kinyume cha sheria.

Jaji wa mahakama hiyo katika uamuzi wake alisema baraza la usalama la nchi hiyo ambalo Rais ni miongoni mwa wajumbe, halina mamlaka ya kupeleka polisi wa kawaida nje ya nchi.

Aliongeza kuwa baraza hilo linaweza kupeleka vikosi vya kijeshi vya ardhini, anga na wanamaji kwa misheni kama hiyo ya kulinda amani nchini Haiti.

Kiongozi wa upinzani, Ekuru Aukot, aliyefungua ombi katika mahakama hiyo, alisema huu ulikuwa ushindi kwa Kenya na kwamba nchi hiyo haiwezi kumudu changamoto za kiusalama kama nchi hiyo ikiwaachilia askari hao.

Aukot alisema Rais William Ruto (pichani) alitaka kukitumia kikosi hicho kwa ajili ya kuimarisha hadhi yake ya kimataifa na kutafuta kupendwa na mataifa ya magharibi kama Marekani.

Kabla ya uamuzi huo, ofisa wa polisi ambaye alizungumza na BBC bila kutajwa jina lake, alisema tayari wamepatiwa mafunzo ya kina ya miezi miwili kwa ajili ya kwenda Haiti.

Mnamo Septemba mwaka jana, Waziri Mkuu wa Haiti, Ariel Henry, alihutubia Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa akitoa wito wa kupelekwa haraka kwa kikosi hicho cha kimataifa.

Alisema serikali yake imezidiwa nguvu na magenge ya kihalifu ambayo yanadhibiti asilimia 80 ya mji mkuu wa Port-au-Prince.

Kenya ilijitolea kuongoza kikosi cha kimataifa na kuahidi kupeleka polisi hao kwa idhini ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

Rais Ruto alisema nchi yake ina rekodi ya kuvutia katika ushiriki wa kusaidia kulinda amani duniani.



Raia wa Palestina wakijaribu kuzima moto katika jengo la Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia wakimbizi wa Palestina (UNRWA) baada ya kushambuliwa juzi. **PICHA: AP**

# Mauaji ya kutisha yazidisha shinikizo Israel kusitisha vita

**GAZA,** PALESTINA

HOFU inazidi kutanda kwa raia wa Kipalestina waliozingirwa na mapigano makali yanayoendelea katika mji wa Khan Younis na kusababisha kuongezeka kwa wito kutoka mataifa mbalimbali wakitaka vita kusitishwa.

Hali hiyo mbaya haipo kwa mji huo pekee, bali katika maeneo mengi ndani ya Ukanda wa Gaza.

Kulingana na Wizara ya Afya inayosimamiwa na kundi la Hamas, karibu watu 26,083 wameuawa katika vita hiyo iliyoanza Oktoba 7, mwaka jana.

Jana pekee wizara hiyo ilisema watu 20 waliuawa na wengine 150 kujeruhiwa, wakati wanajeshi wa Israel wakishambulia walipokuwa wakisubiri kugawiwa misaada katika viunga vya kaskazini mwa Jiji la Gaza.

Mkazi mmoja Abu Ata Basal, aliliambia shirika la habari la AFP kwamba watu walikuwa wakisubiri kupewa chakula,lakini ghafla, vifaru vya jeshi la Israel vikatokea na kuanza kuwafyatulia watu risasi, na miili ya watu ilikatika vipande vipande.

Mwandishi wa habari wa AFP alisema alishuhudia miili ya watu ikiwa imetapakaa sakafuni katika hospitali ya al-Shifa.

Katika taarifa ya Hamas iliyotolewa jana, ilisema tukio hilo lilisababishwa na mashambulizi ya risasi na makombora ni sawa na uhalifu wa kutisha wa kivita.

Hata hivyo, serikali ya Israel haijasema chochote kuhusiana na madai hayo.

Shambulizi hilo limefanyika siku moja baada ya Umoja wa Mataifa kueleza vifaru vya jeshi la nchi hiyo vilishambulia makao makuu yake katika mji wa Khan Younis na kuwaua watu 13.

Nchi ya Ufaransa imeiomba Israel kuheshimu sheria za kimataifa na kuungana na Marekani kulaani shambulizi hilo lililofanyika Khan Younis.

Hata hivyo katika taarifa yake haikutaja moja kwa moja Israel kama muhusika.

Waziri Mkuu wa Uingereza Rishi Sunak,alielezea wasiwasi wake kuhusiana na tishio dhidi ya maisha ya watu wa Ukanda wa Gaza baada ya kituo cha utangazaji cha ITV kurusha picha zilizoonyesha raia aliyeshambuliwa licha ya kuwa na bendera nyeupe mkononi.

Alirudia kutoa wito kwa Israel na Hamas kusitisha mapigano,kuwaachia mateka na kuruhusu uingizwaji wa misaada ya kibinadamu.

"Unajua, Rais Biden alizungumza na mimi kuhusu hili mapema wiki hii. Nimezungumza na Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu kuhusu hili. Na kile tunachotaka kukiona ni kusimamishwa mapigano ili mateka waachiwe na misaada zaidi kuingizwa kwenye Ukanda wa Gaza." Alisema Sunak.

Hamas aidha imeripoti kuwepo kwa mashambulizi makali katikati ya mji wa Khan Younis, ambako kuna makazi ya mkuu wa kundi hilo Yahya Sinwar.

Taarifa kutoka Marekani zilisema mkurugenzi wa Shirika la Ujasusi la nchini Marekani (CIA), William Burns atakutana na wenzake wa Israel na Misri pamoja na Waziri Mkuu wa Qatar ili kufanya mazungumzo ya kusitisha mapigano na kuachiliwa kwa mateka.

Kulingana na vyombo vya habari vya nchi hiyo, Burns atakutana na viongozi hao katika siku chache zijazo.

Gazeti la Washington Post na Axios, katika taarifa zao havikutaja mahali watakapokutana. Hata hivyo, si CIA yenyewe wala Ikulu ya White House waliokubali kuthibitisha taarifa hizo.

Wakato huo huo, Shirika la ndege la taifa la Israel (El Al) limetangaza kusitisha safari za kwenda Afrika Kusini kuanzia mwisho wa Machi kutokana na uhaba wa wateja.

"Kutokana na hali ya usalama ilivyo sasa, kumekuwa na upungufu mkubwa wa mahitaji ya wasafiri wa Israel wanaokwenda maeneo mbalimbali, ikiwemo Johannesburg nchini Afrika Kusini," ilisema El Al katika taarifa yake.

Iliongeza "Kwa kuzingatia hilo, kuanzia mwishoni mwa Machi 2024, tutasimamisha shughuli kwenye njia ya Johannesburg-Tel Aviv."

Tangazo hilo linakuja muda mfupi kabla ya Mahakama ya Kimataifa ya Haki (ICJ) kutoa hukumu katika kesi iliyofunguliwa na Afrika Kusini ikiituhumu nchi hiyo kufanya mauaji ya kimbari Ukanda wa Gaza.

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## TANGAZO LA KUPOTEA KWA MKATABA WA KIWANJA

**JANE PHILIPO MINJA** anatangaza kupotelewa na Mkataba wa Kiwanja namba 274 Kitalu 'A' Kilichopo Mlandizi Disunyara. Kwa yeyote atakayeuona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIN/6914/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MWANAYASU MTUTURA ABDALLAH** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1409/0023** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **HAGAFILO SEKONDARI - NJOMBE** mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/11952/2024.**

**Summons to appear (O.V, R.20 (1) of (Civil Procedure Code)**
**(Substituted Service)**
**IN THE COURT OF TANZANIA DAR ES SALAAM**
**(LAND DIVISION)**
**LAND REVISION NO. 28610 OF 2023**
**RAFAEL YAKOB NDITI.......................APPLICANT**
**VERSUS**
**MOHAMED SALUM CHIBANGO.............RESPONDENT**
**TO: DAGOBERT JOHN KOMBA**
**(THE LEGAL ADMINISTRATOR OF ANSILA KAPINGA)**

**WHEREAS:** The above named **APPLICANT** obtained an REVISION against you. You are hereby summoned to appear in this Court in person or by advocate or authorized Agent on 29th day JANUARY, 2024 at 09:00 AM Before HON. M. GWAE, JUDGE to answer the said REVISION and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your replay.

TAKE NOTICE that, in default of your appearance on that day, the said REVISION will be heard and determined in your absence.

Given under my hand and the seal of this Court, this 25th JANUARY, 2024.

DEPUTY REGISTRAR

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GRACE PHILIP NGUMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 726 EEY aina ya TOYOTA FORTUNER Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIN/10921/2024.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**EMMANUEL ABIUD MWEMBE** Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **SINORAY** yenye usajili namba **MC 254 DCW.** Yenye Chasis namba **LD3PCK6J8M2013117** na Engine namba **21083132** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . Polisi Taafifa : **PHQ/KIL/MOS/1406/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LUCY KALIST KIMARO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA RAV 4** yenye usajili namba **T 501 CZV, CHASSIS NAMBA: ZCA260012979** na ENGINE **NAMBA: 1ZZ0012979.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/ARU/ARU/1990/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GAGI

**GREYSON STANLEY MARISA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA RAV 4 yenye usajili namba T 124 DMX kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **PHQ/ARU/ARU/1938/2024**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**MAJID J. MBALE** anatangaza kupotea kwa kadi mbili za pikipiki, ya kwanza yenye jina JUMANNE RAMADHANI KAZIMBA namba za usajili MC 102 DEG aina ya BOXER. Ya pili yenye jina DEOGRATIUS PETER KAVISHE namba za usajili MC 903 DHH aina ya BOXER. Yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa za Polisi: PHQ/DAR/UBU/11409/2024. Taarifa ya polisi: **PHQ/MOR/MOR/1838/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANNO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TANGA**
**Kituo cha MJINI TANGA Mkoa TANGA**
**Usimamizi wa mirathi Na. 12 /2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU................................MUSSA OMARI SEFU**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA........................ADAMU OMARI SEFU**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5 (2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama ya Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 8 Mwezi 2 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia:**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo tarehe 26 mwezi 01 mwaka 2024

## KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA

**REDMAN LAMECK KAFWIMBA** anatangaza kupotelewa na Ofa ya kiwanja Namba 341 Kitalu 'B' BWIRU Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MWA/ILE/1854/2024.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 765 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**ESTER TRYPHONE RECHUNGURA**
**And**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION OF BY EMMANUEL ADOLPH BALEBI**

**GENERAL CITATION**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.

The matter comes for mention on the 31 day of 1..............................................................2024 before Hon k.Mwanemile-sem at 09:00AM

Dated at Dodoma this 16 day of 1................2024

RESIDENT MAGISTRATE

..................................................................................
**RESIDENT MAGISTRATE**

## KUPOTEA KWA CHETI



**NURU J. MAIRI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S3933-0014 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia RISING STAR SECONDARY SCHOOL mwaka 2018. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/MWA/NYA/11142/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOHN RAMSAY KINLOCH** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0729-0067 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MSOLWA SEKONDARI mwaka 2005. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/11341/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **OMARY SAIDI MWADINI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya King lion yenye namba za usajiri MC 710 DKD, Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu nae.Taarifa ya Polisi: **PHQ/TAN/611/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**BEDSON JOHN DAVID** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC 210 BZE aina ya SANLG rangi Nyekundu, Chassis No.LBRSPJB51J9021886. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/11469/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SELEMAN HAMIS** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S3857 – 0052 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia NGOGWA SECONDARY SCHOOL mwaka 2012. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: MAS/RB/1465/2021**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**MARTIN NTWINA GERFRID** Anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria(passport) yenye namba TAE447807 iliyotolewa na ofisi ya uhamiaji, kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**PHQ/MOR/MOR/1653/2024**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**LILILOKO DODOMA**
**MAOMBI MADOGO NA. 286 YA MWAKA 2023**
**NELSON ADAMSON ...................................... MDAI**
**VERSUS**
**YUDITH MYEYA .................................... MDAIWA**
**KWA:**
**YUDITH MYEYA**
**POPOTE ULIPO**
**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 06.02.2024 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

ANGALIZO: Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu. Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya wito, baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 12 ya mwezi wa Desemba,2023

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

KENNEDY ALISON MTWALE anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T 848 DLB aina ya MERCEDES BENZ, Chassis No. WDD2040412R025432, Engine No. 27195031022525. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya Polisi: PHQ/DOD/DOD/2563/2024

## KUPOTEA KWA VYETI



**RIDHIKI SALUMU NJAKULA** anatangaza kupotea kwa vyeti. NTA LEVEL 4 Basic Techinician Certificate in Human Resource Management chenye Registration No. BTCHRM 18/03/M 505 kilichotolewa na TANZANIA PUBLIC SERVICE COLLEGE (TPSC) MTWARA May 10 2019. NTA LEVEL 5 Technician Certificate in Human Resource Management chenye Registration No. DHRM 03/19/MTW 851 kilichotolewa na TANZANIA PUBLIC SERVICE COLLEGE (TPSC) MTWARA mwaka 2020. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MTW/NEW/RB/729/2022.**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MWANTUMU, au mama Mwadawa, ni mwanamke ambaye muda wote yeye anachowaza ni umbea, ugomvi na kufitinisha watu.

Anawagombanisha majirani wasielewane, ndoa za majirani zake nazo haziko salama hajaziacha, kwani amekuwa akizitikisa.

Kwa bahati mbaya au nzuri anaishi kwenye nyumba ya urithi ya marehemu mama yake, yeye akiwa ndiye mama mwenye nyumba.

Cheo hicho cha Umama wa Nyumba asiyojenga, ndiyo akawa amepata fimbo ya kuwapigia watu.

Wapangaji wanaopanga kwenye nyumba hiyo wamekuwa wakiishi kwa amri, manyanyaso, kufokewa kama watoto wadogo. Ndani ya nyumba hiyo, wapangaji wamekuwa kama wakiishi bure au kwa mama wa kambo, huku silaha yake kubwa ikiwa ni kuwatishia kuwahamisha. Hebu fuatilia mwanzo na mwisho wa visa vya mama huyu.

# Mama mwenye nyumba-12

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

Akatoka nje. Hakuwa peke yake. Mkononi alikuwa amemshika mwanaume mmoja mwenye umri unaokadiriwa kufikia au kukaribia miaka 30 hivi, aliyevaa shati jeupe na suruali ya jeans nyeusi na viatu aina ya raba rangi ya bluu.

Ile kutoka tu, umati ulipiga kelele ambazo zilikuwa za aina tofauti. Wengine walikuwa wanashangilia na wengine kuzomea. Zote zilitoka kwa wakati mmoja na kusababisha kelele zisizokuwa na mpangilio.

Kwanza zilizuka vurumai, Devota akitaka kwenda kumpiga mumewe, lakini alidhibitiwa na askari.

"Mama ndiyo huyu mumeo?" Akauliza Mwenyekiti wa Serikali ya Mitaa Magomeni Mikumi.

"Ndiyo, na anatembea na binti wa mama mwenye nyumba yangu, kuwadi ni mama yake mwenyewe."

"Mbona hammtoi huyo fisadi kiwembe mchukua mume za watu?" Akapiga kelele Tabia, mpangaji mwenzake Devota.

Na hilo ndilo kama lilikuwa swali la wengi, ambao walitaka msichana aliyekuwa naye mle nadhani naye atolewe, wote wapelekwe kituoni.

"Sisi tunaiwakilisha serikali, mle ndani yule binti ametuambia amechiwa chumba na rafiki yake ambaye amekwenda kwenye msiba wa mama yake mdogo.

Ndugu wananchi tunachofanya hapa ni kumchukua huyu bwana kwa usalama wake, tunampeleka sehemu ya usalama kwa sababu bado kuna watu wana hasira naye akiwemo mkewe.

Binti yeye siyo kama tumemuacha, ila kwa busara tumeona tumuachie aendelee kulinda chumba cha mwenzake, kwa sababu kama tukimchukua halafu kukatokea kitu chochote kibaya, ikiwemo wizi, ataingia kwenye matatizo wakati ana matatizo mengine. Tumemuacha kwa muda, akirudi mwenzake tumemwambia aripoti kwanza kituoni, mengine yatafuata baadaye." Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa alitoa ufafanuzi.

************************************

"Nasema hivi, naondoka, na kwenda kwa shangazi yangu Kawe. We bwana kumbe muuaji. Sisi tunagombana na mama mwenye nyumba, wewe kumbe ni mkweo.

Haya baba nakuacha na 'mkeo' huyo uliopewa na mama mkwe wako."

Devota alikuwa akizungumza huku akikusanya kilicho chake akiamua kuondoka baada ya sakata la kumfumina mumewe




**"Mwanangu kaniheshimisha. Bado hawa wawili nao watanitambua, mimi ndiyo Mwantumu au mama Mwadawa," alijipongeza kimoyomoyo.**

akiwa chumbani na binti wa mama mwenye nyumba wake.

"Na ukija kwa shangazi sitaki chochote, ila talaka yangu tu. We mwanaume huna haya wala huoni vibaya, yaani mimi kwenda kunichanganya na kile kitoto kweli?

Kitu gani nilichokukosea au nini ambacho umekikosa kwangu hadi kunidhalilisha kiasi hiki?

Si kunidhalilisha huku! Kili kichokuvutia kwake, au ndiyo mama kwenye nyumba kakwambia ukimchukua ndiyo utakuwa huhami?" Yalikuwa na malalamiko ya uchungu kutoka kwa Devota.

Wakati huo Peter, mumewa Devota alikuwa kimya. Alikuwa mdogo kama punje ya choroko. Kitu alichokutana nacho hakutegemea. Hakuwahi hata siku moja kufumaniwa.

Tamaa ya kuwa na msichana mdogo kama Mwadawa au Amina ilimponza. Leo hii eneo zima linajua kama amefuminia.

Kwanza kilichomshangaza ni umati wa watu uliomiminika kwenye fumanizi lake wakubwa na wadogo ilikuwa ni kama walialikwa, au tangu alivyokuwa akichati na Mwadawa walikuwa wanajua kinachoendelea.

Kitu ambacho alishindwa kuelewa kuwa mkewe alikuwa na ramani yote ya vita. Kila alichokuwa akichati na mpenzi wake mpya, Mwadawa, mkewe alizifuma meseji na kuweka mkakati kabambe wa fumanizi.

Na alipowaambia mashoga zake, nao wakawambia wenzao, kwa hiyo ni kama vile watu walikuwa wamelikwa kwenye ngoma.

Walijua ni eneo gani, saa ngapi na wanakwenda kufumaniwa ni nani na nani. Waliingia kwenye mtego kirahisi sana.

Wakati Devota akiamua kwenda Kawe kwa shangazi yake, Mwadawa yeye baada ya shoga yake Zao kurejea kwenye msiba namkabidhi chumba chake hakuridi nyumbani kwao.

Akakimbilia Gongolamboto kwa mjomba wake. Angeweka wapi sura yake. Binti mdogo kama yule kuchukua waume za watu ilikuwa ni stori kubwa.

Kwa upande wa Mwantumu yeye lengo lake lilikuwa limetimia. Kumkomoa Devota ilikuwa ni lengo lake. Na kumfanya asononeke kwa kuchukuliwa mume ni jambo lililomfurahisha zaidi kuliko kiti kingine chochote.

Ni mmoja kati ya watu wachache ambao wala hawakusikitika na lile fumanizi. Ndiyo kwanza alilishangilia. Alimuona binti yake kama ni shujaa na aliyemlipia kisasi mama yake bila yeye mwenye kufahamu.

"Mwanangu kaniheshimisha. Bado hawa wawili nao watanitambua, mimi ndiyo Mwantumu au mama Mwadawa," alijipongeza kimoyomoyo.

Peter hakurejea tena nyumbani kwa Mwantumu. Haikujulikana kaenda wapi! Haikujulikana kama amemfuata mkewe Kawe au na yeye ameamua kutorudi nyumbani kwa ajili ya aibu.

Akimpigia simu hapokei. Akampigia binti yake Mwadawa Gongolamboto na kumuuliza kama anawasiliana na Peter.

"Mama tangu siku ile ya fumanzi sijaonana naye tena. Na nikimpigia simu wala hapokei."

"Kama mimi tu, nikimpigia simu hapokei, kumbe hana maana mwanaume huyu! Yaani kafumaniwa, hajapigwa, wala hajashtakiwa, amekuwa mwoga kama kunguru."

"Yaani mama ilikuwa nataka kumpigia nimwambie sasa hivi kama akitaka tukutane juu kwa juu na siyo huko tena lakini hapokei, lakini tusilaumu sana labda haipo mikononi mwake," Mwadawa alimjibu mama yake.

"Na huyo cha ukorofi nasikia yuko Kawe na Shangazi yake, eti anaomba talaka, ataenda wapi mbwa yule, ngoja tu nifanye uchunguzi wangu nitajua tu nini kinaendelea."

"Mama na hicho chumba je?" Mwadawa akauliza.

"Nataka niende kwa mjumbe aje tukifungue kama kuna viti vimebaki vikusanywe vihifadhiwe nipangishe, na hawa waliobaki Tabia na Rozi nimeshaanza kuwaambia madalali waanze kutafuta wapangaji. Hapa mwanangu miezi miwili ijayo tutakuwa na wapangaji wapya kabisa, mbona nitanenepa mama yako, maana nimechoshwa na hii mingurumbembe."

"Ila na wewe mama acha umbea na maneno maneno, hao nao wakija ukigombana nao utaonekana una hila."

"Umeanza na wewe, kama huna la kusema kata simu hiyo."

Yalikuwa ni mazungumzo wa simu ya mtu na binti yake. Mwantumu na binti yake Mwadawa.

Mwantumu akiwa nyumbani kwake, Mwadawa kwa mjomba wake Gongolamboto wakipeana dondoo na kile kichotokea siku ya fumanizi na nini kinaendelea baada ya hapo.

Wapangaji waliobaki Rozi na Tabia ni kama walibaki wakiwa. Kitendo cha Devota kuondoka ilikuwa pigo kubwa kwao.

Pamoja na hayo hata wao walikuwa karibuni kuondoka kwenye nyumba hiyo. Ila, awali walipatana kuwa hata wakihama, watakapopata nyumba za kuhamia, angalau wasiwe mbalimbali sana na wala wasihamie mbali sana na pale.

Lengo ni kuendeleza vita nyingine na Mwantumu, mama mwenye nyumba wao kwa sasa.

Walijua kuwa watakapokuwa nje ya utawala wa nyumba yake, watampelekesha kweli kweli.

Kama tu wapo kwenye nyumba yake na wanamkosesha usingizi, basi watakapokuwa wamepanga sehemu nyingine, hawatotishika na amri zozote za umama mwenye nyumba, badala yake atakuwa kwao ni mtu wa kawaida tu.

Katika mazungumzo yao, Tabia ya Rozi wakaamua kumfuata Devota Kawe kuongea naye kwa jambo moja tu, la kulipiza kisasi cha mama mwenye nyumba wao.

ITAENDELEA JUMAMOSI

# BIASHARA UNITED, PAMBA FC VITANI CHAMPIONSHIP

**Na Oliver Albert**

KOCHA Mkuu wa Biashara United, Amani Josiah, amesema kikosi chake hakina presha yoyote kuelekea mechi ya Ligi ya Championship dhidi ya Pamba FC itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini, Mwanza.

Timu hizo kutoka Kanda ya Ziwa zimeonyesha upinzani mkali, zikiwa zinafukuzana katika msimamo wa ligi hiyo, Pamba ya Mwanza ikiwa ya pili na pointi 40 kibindoni wakati Biashara United ya Mara iko nafasi ya tatu ikiwa na pointi 37.

Vinara wa ligi hiyo ni Ken Gold ya jijini, Mbeya yenye pointi 42 ambapo leo itashuka kuumana na 'ndugu' zao Mbeya Kwanza kwenye Uwanja wa CCM Sokoine Mbeya.

Akizungumza na gazeti hili jana, Josiah alisema kikosi chake kimejipanga vyema na anaamini wataibuka na ushindi na kukaribia malengo yao.

Kocha huyo alisema anajua mchezo huo utakuwa mgumu kutokana na ubora wa wapinzani wao lakini wamejiandaa kuwakabili ili wapate ushindi na kukaa kileleni.

“”Tuko vizuri na hata nafasi tuliyopo sasa hatujafika kwa bahati mbaya, imetokana na kumepambana sana katika mechi zilizopita.

Sina presha na mechi dhidi ya Pamba labda wao ndio watakuwa ana presha kwa sababu wanacheza nyumbani, lakini sisi tumejiandaa vizuri kuwakabili ili kuondoka na ushindi,” alisema Josiah na kuongeza;

“Ligi ni ngumu na mapambano ni makali ndio maana unaona timu nyingi hata pointi hatujapishana sana, hivyo lazima tujipange vizuri kila mechi na ukizingatia huu ni mzunguko wa lala salama.”

Biashara United imekuwa katika kiwango bora katika Ligi ya Championship ikionyesha imepania kurejea tena kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kushuka daraja mwaka 2022.

Timu hiyo iko katika vita kali ya kupanda ikichuana na Kengold, Pamba, Mbeya Kwanza, TMA, Mbuni na Mbeya City.




Meneja wa wateja maalum wa Tigopesa, Mary Ruta (kushoto) akimkabidhi mfano wa hundi ya shilingi milioni moja mshindi katika droo ya Magift dabodabo, Kumbuka Mbugulu jijini Dar es salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mchoma nyama mshindi magifti

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Dar es Salaam, Novat Lyaruu, ambaye anajishughulisha na biashara ya uchomaji nyama jana alitangazwa kuwa mmoja wa washindi wa Sh. milioni moja katika droo ya tisa ya Promosheni ya Magifti Dabadabo inayoendeshwa na Kampuni ya Tigo.

Mbali na Lyaruu, Kumbuka Mbugulu na Jenifer Gunga, pia waliibuka washindi na kukabidhiwa zawadi zao kwenye ofisi za kampuni hiyo jijini.

Akizungumza baada ya kuwakabidhi washindi hao mfano wa hundi za fedha, Meneja wa Wateja Maalum wa Tigo Pesa, Mary Rutha, amewasisitiza Watanzania kuendelea kufanya miamala mbalimbali na Tigo Pesa ili kujiweka katika nafasi ya kuibuka washindi wa fedha, vifaa vya Hisense na zawadi kubwa ya magari mawili katika droo mbilii zilizobakia.

“Desemba Tigo tuliwapeleka washindi 15 Dubai, na wengine walienda Zanzibar katika kampeni hii hii, wapo pia waliojishindia pesa na vifaa vya Hisense. kwa hiyo kampeni bado inaendelea na tumebakisha droo mbili, wateja waendelee kufanya miamala ili kushinda,” alisema Mary.

Kwa upande wa washindi, Lyaruu alisema fedha aliyopata atanunua mbuzi wa kutosha na kuongeza mtaji wake huo wa kuchoma nyama.

“Pesa hizi zitaongeza mtaji wangu, nitaongeza mbuzi zaidi, kwa kweli nimefurahi sana,” alisema Lyaruu.

Jenifer ambaye ni mkazi wa Kisarawe, Pwani alisema alikua na ndoto ya kufungua saluni hivyo fedha aliyopata itafanya ndoto yake hiyo kutimia.

## Kikapu Zanzibar waahidi mageuzi

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Mpira wa Kikapu Zanzibar (BFZ), limesema linajipanga kuendesha mashindano mbalimbali ya mchezo huo visiwani hapa yenye lengo la kuongeza hamasa na ladha kama ilivyo michezo mingine, imeelezwa.

Rais wa BFZ, Abdullatif Ali Yasin, katika taarifa yake iliyotolewa na Ofisa Habari wa shirikisho hilo, Hussein Karama, amesema ni lazima mpira wa kikapu uchezwe Zanzibar ili kuleta hamasa na kukuza vipaji vilivyopo.

Kiongozi huyo alisema kwa muda wa miaka miwili hakuna ligi yenye usimamizi mzuri iliyochezwa visiwani humo na ndio sababu mojawapo ya Baraza la Michezo la Zanzibar (BMZ), iliamua kuteua viongozi wa muda ili kusimamia kikapu na hatimaye kufikia malengo.

Karama alisema anaamini kwa ushirikiano wa pamoja kati ya viongozi na wadau wa michezo wenye uzoefu watafikia malengo yaliyokusudiwa.

Alieleza kufanyika kwa mashindano ya kipau ya Kombe la Mapinduzi ilikuwa ni mwanzo na sasa wanajipanga kuhakikisha michuano yote iliyotajwa kwenye kalenda yao inachezwa.

“Kikapu ili kionekane ubora wake ni lazima kichezwe kwanza, tumeona tuanze na Ligi ya Mapinduzi, tukitoka hapa tusimamia Ligi Kuu, Taifa CUP (Kombe la Taifa) na Karume Cup (Kombe la Karume),” alisema kiongozi huyo.

Alieleza mashindano yote hayo yakifanyika katika ubora wake, vijana watapata nafasi ya kuonyesha uwezo wao na vile vile kucheza idadi kubwa ya mechi ambazo pia zitawasaidia katika kuunda timu ya taifa yenye ubora.

“Kwa pamoja tukiwamo sisi wasimamizi na viongozi, wachezaji, wadau lakini na viongozi wa serikali, wananchi kwa ujumla tukishirikiana, tutafikia makusudio yetu,” Karama aliongeza.

Bosi huyo alisema jambo lolote ambalo halisimamiwi vizuri, wahusika wanaweza kukata tamaa lakini sasa wanaomba kuungwa mkono ili kusimamia vyema mchezo huo na endapo itatokea hitilafu watakuwa tayari kukosolewa na kurekebishwa kwa ajili ya nia kuujenga mchezo ifikiwe.

Aliongeza katika kuhakikisha mipango hiyo inafanikiwa, BFZ inahitaji fedha ambazo zitasaidia shughuli za uendeshaji huku pia wadhamini wakitakiwa kujitokeza kuzibeba klabu ambazo zinahitaji kuwawekea wachezaji mazingira mazuri.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### NEWCASTLE KUMUUZA WISON

KLABU ya Newcastle United inaweza kumuuza mshambuliaji wa England, Callum Wilson mwenye umri wa miaka 31 kwa pauni milioni 18 pekee katika wiki ya mwisho ya dirisha la uhamisho la Januari, huku Chelsea, Arsenal na Manchester United zote zikiwa zimejulishwa kuhusu kupatikana kwake. **(Standard)**

### DURAN KUTUA CHELSEA

CHELSEA ni miongoni mwa klabu zinazotaka kumsajili mshambuliaji wa Aston Villa na Colombia, Jhon Duran mwenye umri wa miaka 20, kabla ya tarehe ya mwisho ya usajili. (Sky Sports)

### HAG ATAKA NYOTA MAN

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag anamtaka mshambuliaji wa Ajax na Uholanzi, Brian Brobbey na mlinzi wa Everton, Jarrad Branthwaite, wote wakiwa na miaka 21, lakini Mholanzi huyo hana udhibiti wa kuamua ni mchezaji gani anaweza kusajiliwa. **(Mirror)**

### GIBBS-WHITE AFUATILIWA

KLABU ya Newcastle United inamfuatilia kwa karibu mshambuliaji wa Nottingham Forest, Morgan Gibbs-White mwenye umri wa miaka 23 ili kumsajili katika uhamisho wa Januari hii. (Football Insider)

### WOLVES WANASITA KWA BROJA

KLABU ya Wolverhampton Wanderers inasitasita katika kutaka kumnunua mshambuliaji wa Chelsea na Albania mwenye umri wa miaka 22, Armando Broja kwa pauni milioni 30 huku wakijitahidi kuhakikisha wanazingatia sheria za matumizi ya fedha ya Ligi Kuu England. **(Mail)**

### CARSLEY ATAJWA IRELAND

CHAMA cha soka cha Ireland kina matumaini ya kumwajiri kocha wa England chini ya umri wa miaka 21, Lee Carsley mwenye miaka 49, kuwa kocha mkuu wa Jamhuri ya Ireland. (Independent)

### ANCELOTTI AMTAKA BENZEMA

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti ameiomba klabu hiyo kumsajili tena mshambuliaji wa Ufaransa, Karim Benzema mwenye umri wa miaka 35 kutoka klabu ya Al-Ittihad ya Saudi Aarabia. **(Sport - in Spanish)**

### ROGERS ANAITAKA VILLA

MORGAN Rogers anaaminika kutaka kujiunga na Aston Villa baada ya Middlesbrough kukataa ofa mbili kutoka kwa timu hiyo ya Ligi Kuu ya England kwa ajili ya mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 21. **(Mail)**

### MAPPE BADO HAJAAMUA

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 25, amepokea ofa ya kujiunga na Real Madrid kama mchezaji huru msimu wa joto na nyingine ya kuongeza mkataba wake na Paris St-Germain, lakini bado hajaamua kuhusu mustakabali wake. **(ESPN)**

### PALACE YAMTAKA MUNOZ

KLABU ya Crystal Palace inakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili beki wa kulia wa Colombia, Daniel Munoz mwenye umri wa miaka 27 kutoka kwa Genk ya Ubelgiji.**(South London Press)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MBAPPE AFIKIRIA OFA YA REAL MADRID NA PSG

●●● Nyota huyo bado hajaamua afanye maamuzi gani kutokana na ofa hizo ambazo...

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe amepokea ofa ya kujiunga na Real Madrid kama mchezaji huru msimu ujao na nyingine ya kuongeza mkataba na klabu yake ya sasa ya PSG, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa bado hajaamua juu ya mustakabali wake, kwa mujibu wa ESPN.

Chanzo kimoja kiliiambia ESPN kwamba Madrid wanataka jibu la uhakika kutoka kwa Mbappe katika wiki zijazo ili kumpata msimu wa 2024-25, lakini vyanzo vingine vya karibu na mshambuliaji huyo vinasema hana tarehe ya mwisho ya kufanya uamuzi.

Mbappe, ambaye mkataba wake na PSG unamalizika mwishoni mwa msimu huu, tangu Januari Mosi amekuwa huru kufanya mazungumzo na klabu nyingine.

Madrid wamejaribu na kushindwa kumsajili Mbappe katika misimu ya hivi karibuni, na vyanzo vimeiambia ESPN kwamba ofa ya mkataba wa Madrid wakati huu ni ndogo kuliko ile waliyotoa hapo awali.

Hata hivyo, vyanzo vingine vilisema ofa hiyo bado itamfanya kuwa mchezaji anayelipwa zaidi klabuni hapo.

Chanzo kimoja kiliiambia ESPN kwamba Madrid haitatoa fedha nyingi kama ilivyokuwa tayari hapo awali, huku klabu hiyo ikiwa haitaki kumlipa zaidi ya nyota mashuhuri kwenye kikosi kama vile Vinícius Júnior na Jude Bellingham, ambao vyanzo vilisema wanalipwa karibu euro milioni 10.5 kwa msimu.

Mbappé anapokea euro milioni 37 kwa msimu katika klabu ya PSG na amepewa mshahara sawa na ofa ya mkataba mpya wa klabu hiyo.

Liverpool pia imekuwa ikifuatilia hali ya mkataba wa Mbappe katika miaka ya hivi karibuni.

Mapema mwezi huu, ESPN iliripoti kwamba mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa hajakataa kuhamia Ligi Kuu ya England.

Vyanzo vilivyoshauriwa na ESPN vilisema kwamba wachezaji wengine huko Madrid wana matumaini juu ya nafasi ya Mbappé ya kusajiliwa na klabu katika msimu wa joto, lakini wanakumbuka kuwa na matumaini vile vile kwa mchezaji huyo kurekebisha masharti na PSG.

Licha ya kukatishwa tamaa kwa Mbappé kukataa kusaini Madrid mwaka 2022, chanzo kingine kilisisitiza kuwa rais wa Madrid, Florentino Pérez anaongoza mazungumzo mwenyewe wakati huu na hajawahi kuacha kuwasiliana na mchezaji huyo.

# MO SALAH: NITAPAMBANA KUREJEA AFCON

**LIVERPOOL, England**

MOHAMED Salah ameanza matibabu ya msuli wake wa paja na kusema kwamba, atafanya kila awezalo kuungana tena na Misri kwenye michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika, Afcon.

Salah alirejea Liverpool siku ya Jumatano kwa ajili ya matibabu ya jeraha alilopata wakati Misri ilipotoka sare ya 2-2 na Ghana wiki moja iliyopita.

"Jana (juzi) nilianza mpango wa matibabu na urejesho na nitafanya kila linalowezekana kuwa tayari haraka iwezekanavyo na kurejea timu ya taifa kama ilivyokubaliwa tangu mwanzo," aliandika Salah kwenye ukurasa wake wa Instagram.

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp pia amesema kuwa Salah bila shaka atarejea Afcon iwapo atapona kwa wakati kutokana na jeraha na iwapo Misri itatinga fainali.

Kocha msaidizi wa Liverpool, Pepijn Lijnders alisema Salah anatarajiwa kurejea uwanjani baada ya wiki tatu hadi nne iwapo hakutakuwa na vikwazo katika kupona kwake.

Hata hivyo, fainali ya Afcon imepangwa kufanyika Februari 11 mwaka huu.

"Misri na Liverpool zote zina nia sawa, tunataka Mo Salah awe fiti haraka iwezekanavyo," alisema Klopp akiiambia beIN SPORTS baada ya timu yake kutinga fainali ya Kombe la Ligi kwa kuitoa Fulham Jumatano.

"Iwapo atabaki Afrika na hawawezi kufanya matibabu yanayostahili, itachelewesha kila kitu hasa kwa Misri iwapo watafika fainali.

"Tunamleta hapa sio kwa sababu tunataka kumchukua kutoka Misri, lakini tu kutoa matibabu bora zaidi.

"Yote yamekubaliwa. Ikiwa Salah yuko fiti na Misri kwenda fainali, ilikuwa wazi kila mara, tunataka arudi akiwa fiti kwa asilimia 100, tunataka hivyo."

Misri ambao ni mabingwa mara saba wa Afcon walimaliza nafasi ya pili katika Kundi B wakiwa na pointi tatu baada ya sare tatu mfululizo.

Watacheza na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo katika hatua ya 16 bora kesho Jumapili.

Klopp pia aliwakosoa wale wanaomshutumu Salah kurejea England kwa matibabu, baada ya baadhi wachezaji wa zamani wakisema kwamba kama nahodha alipaswa kubakia kwenye kikosi cha Misri.




# Kufuzu kwa Congo 16 bora kuna maana kubwa - Kakuta

**KORHOGO, Ivory Coast**

KUFUZU hatua ya mtoano ya 16 bora ya michuano ya mataifa ya Afrika, Afcon, kunamaanisha mengi kwa watu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, kwa mujibu wa mlinzi wa timu hiyo, Gael Kakuta.

Kakuta alitwaa tuzo ya mchezaji bora wa mchezo katika suluhu na Tanzania katika pambano la Kundi F kwenye Uwanja wa Amadou Gon Coulibaly, mjini Korhogo.

"Siku zote ni vizuri kupata kombe. Muhimu ni sifa na hii ni nzuri kwa watu wetu wa nyumbani ambao tunajua wamekuwa nyuma yetu katika safari hii ngumu.

"Tulikuwa na kundi gumu lenye timu imara, lakini bidii na sapoti kutoka kwa watu wetu ilitufikisha hapa," alisema Kakuta.

Beki huyo anayekipiga Ufaransa katika Klabu ya Amiens SC alipongeza mchezo mzuri wa Tanzania, ambao wametolewa baada ya kumaliza mkiani mwa kundi hilo.

Licha ya kutofuzu, ni taifa zuri sana linaloendelea. Kwa kweli walitupa sisi na kundi lingine kazi kubwa ya kufanya.

"Kwa sasa, tutafurahia wakati huu. Hawakufunga na hiyo ni ishara chanya ambayo tunaweza kuifanyia kazi," aliongeza Kakuta.

# Ivory Coast yakwama kumwazima kocha Renard

**ABIDJAN, Ivory Coast**

IVORY Coast imeshindwa kumpata kocha Hervé Renard kwa mkopo kutoka timu ya taifa ya Wanawake ya Ufaransa kwa muda uliosalia wa Kombe la Mataifa ya Afrika, Afcon.

Renard aliiongoza Ivory Coast kunyakua taji hilo mwaka 2015 na shirikisho la soka nchini humo lilikuwa na nia ya kumrejesha kwa jaribio lingine baada ya kumtimua kocha wake mkuu, Jean-Louis Gasset.

Lakini mazungumzo na Shirikisho la soka la Ufaransa kuhusu uwezekano wa mkataba wa mkopo kwa Renard yalivunjika bila makubaliano Alhamisi.

"Mazungumzo hayakuisha vyema, ni kwa sababu haikupaswa,"alisema Renard mwenye umri wa miaka 55 akiiambia chaneli ya Canal Plus. "Ningeipenda, lakini hatima ilichagua vinginevyo."

Ivory Coast ilishindwa kufuzu moja kwa moja kwa hatua ya mtoano wa timu 16 ilipofungwa 4-0 na Equatorial Guinea katika mchezo wao wa mwisho wa kundi Jumatatu, lakini walipata nafasi ya kusonga mbele kama mmoja wa washindi wanne bora wa nafasi ya tatu, 'best looser'.

Ivory Coast hatimaye ilifuzu kwa hatua ya 16 bora Jumatano -- baada ya Gasset kutimuliwa, shukrani kwa ushindi wa Morocco dhidi ya Zambia.

Kocha wa muda Emerse Faé huenda akasalia kuwa kocha kwa ajili ya mchezo dhidi ya bingwa mtetezi Senegal mjini Yamoussoukro Jumatatu.

Shirikisho la Soka la Ivory Coast halijazungumza hadharani kuhusu suala hilo.

Renard bado ni maarufu nchini Ivory Coast kwa kuiongoza nchi hiyo kutwaa taji lao la pili la Kombe la Afrika.

Kocha huyo hilo lilikuwa taji lake la pili la Afrika baada ya kuiwezesha Zambia kulitwaamwaka 2012.

Aliiongoza Saudi Arabia kuwafunga Argentina kwenye mchezo wa kwanza wa kundi kwenye kombe la Dunia mwaka 2022, kabla ya kupewa mikoba ya kuinoa timu ya taifa ya Wanawake ya Ufaransa mwaka jana.

# MSHAMBULIAJI MPYA SIMBA ATOA NENO, ATARAJIA MAZURI

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI mpya wa Wekundu wa Msimbazi, Fredy Michael, ametaka ushirikiano kutoka kwa kila mtu ndani ya timu hiyo na anaamini hali hiyo itawasaidia kufikia malengo yao kwa haraka.

Fredy aliambia gazeti hili amefurahi kujiunga na Simba na yupo tayari kuhakikisha anaisaidia kufanya vizuri katika michezo iliyopo mbele yao ikiwamo Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la FA na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Nyota huyo tayari amewasili nchini ikiwa ni mara yake ya kwanza kutua Tanzania, ni miongoni mwa wachezaji watano wapya waliosajiliwa na Simba kipindi cha dirisha dogo, wengine ni Babacar Sarr, Saleh Karabaka, Ladack Chasambi na Edwin Balua.

Akizungumza na Nipashe jana, nyota huyo alisema ni ngumu kwa mchezaji mpya kuingia ndani ya timu na kupata nafasi katika kikosi cha kwanza haraka lakini anaamini kwa ushirikiano atakaoonyesha kwa wachezaji wenzake na kiwango alichonacho atamshawishi kocha Benchikha (Abdelhak) kumpanga.

"Kikubwa ni ushirikiano kutoka kwa kila mtu ndani ya klabu ikiwamo wachezaji wenzangu, nipo tayari kuipambania timu kusaidia kufikia malengo ambayo yanayotarajiwa.

Ninaimani kubwa ya kufanya vizuri na kukata kiu ya mashabiki, kutowaangusha, kocha na viongozi walinisajili kwa ajili ya kuhitaji huduma yangu ili kufikia kile ambacho wanakitarajia katika mashindano mbalimbali yaliyopo mbele yao," alisema Fredy.

Naye Kocha Msaidizi wa Simba, Seleman Matola, alisema wachezaji wote ambao hawako katika majukumu ya Timu za Taifa pamoja na nyota wapya wameshawasili kambini ili kuanza mazoezi rasmi kwa ajili ya maandalizi ya michezo iliyopo mbele yao.

Matola alisema walianza na mazoezi ya gym baada ya kushindwa kwenda uwanjani kutokana na mvua kubwa kunyesha Dar es Salaam, na sasa wanaendelea na programu nyingine zilizotolewa na benchi la ufundi ambazo zinalenga kuwaimarisha.

"Tumeshaanza mazoezi kwa ajili ya kujiweka tayari kuelekea mechi za Ligi Kuu, Kombe la FA na michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, nyota wote wako kambini isipokuwa walioko kwenye Timu za Taifa, lakini tunatarajia hivi karibuni nao wataungana na klabu hasa kwa zile timu ambazo zimetolewa AFCON," Matola alisema.



Mchezaji wa timu ya Vijana raia wa Congo DRC,Tony Pierre, akimruka mchezaji wa timu ya vijana wanaolelewa na Kituo cha michezo cha Jakaya Kikwete (JKPARK), Salum Ibrahim, wakati wa mchezo wa kirafiki uliopigwa kwenye viwanja vya kituo hicho jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ligi ya Wanawake kumekucha

**Na Saada Akida**

NYASI za viwanja vinne zitawaka ‚moto' wakati vita ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake Tanzania itakapoendelea ambapo Simba Queens itawaalika Alliance Girls kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Mabingwa watetezi wa ligi hiyo, JKT Queens, wao watakuwa ugenini kukabiliana na wenyeji, Fountain Gate Princess kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma.

Michezo miwili itakayopigwa leo ni kati ya Ceasiaa Queens dhidi ya Baobab Queens kwenye Uwanja wa Samora, Iringa huku Amani Queens ikiwakaribisha Geita Gold Queens kwenye Uwanja wa Ilulu, Lindi.

Kocha Msaidizi wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', alisema baada ya kutoka sare dhidi ya Bunda Queens, walirejea kwenye uwanja wa mazoezi kufanyia kazi makosa yao na sasa wako tayari kupata ushindi.

"Haitakuwa mechi rahisi, tunaenda kupambana na kusaka alama tatu muhimu ili kujiweka katika mazingira mazuri katika malengo yetu kwenye mbio za ubingwa na kurejesha heshima ya Simba," alisema Mgosi.

Naye Kocha Mkuu wa Alliance Girls, Ezekiel Chabanka, alisema wamewasili Dar es Salaam salama na wachezaji wake wapo tayari kuwakabili wapinzani wao wakipanga kuvuna pointi tatu dhidi ya timu hiyo ‚kubwa' yenye wachezaji wazoefu.

"Tumekuja kuonyesha ushindani, tunafahamua ubora wa Simba Queens ikiwamo kuwa na wachezaji wenye uzoefu kuliko timu yangu, lakini ninaimani kubwa ya kucheza mchezo mzuri ," alisema Chabanka.

Kocha wa JKT Queens, Esther Chabruma, alisema wachezaji wake wapo tayari kwa ajili ya mchezo wa leo dhidi ya Fountain Gate Princess na wanataka kuendelea pale walipoishia katika michezo iliyopita.

## Simba, Yanga, Azam zageukia FA Cup

INATOKA UK. 24

"Tumetolewa kwenye AFCON hatukupata bahati ya kwenda kwenye raundi ya 16 bora, kwa hiyo unaweza kuiona Ligi Kuu imebaki na wachezaji watatu tu AFCON, hivyo inaweza kuendelea," alisema.

Wachezaji wanaocheza Ligi Kuu Tanzania Bara waliobaki AFCON baada ya timu zao kusonga mbele ni, Stephane Aziz Ki wa Yanga kwenye kikosi cha Burkina Faso, Djigui Diarra wa Yanga anayecheza timu ya Mali, na Henock Inonga wa Simba ambaye yupo kikosi cha Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Ratiba ya 16 bora ya AFCON inaonyesha nyota wa Ligi kuu, Diarra na Aziz Ki watakutana uso kwa uso kwenye hatua hiyo wakiwa na vikosi vyao katika mchezo wa hatua hiyo.

Nyota wa Simba, Inonga akiwa na timu yake watacheza na timu ya taifa ya Misri kuwania kutinga hatua ya robo fainali.

## Musonda arejea kuipa Yanga ubingwa

INATOKA UK. 24

nao ni wale wale ambao tunakutana nao mara kwa mara kwenye Ligi ya Mabingwa na hata msimu uliopita kwenye Kombe la Shirikisho," alisema Mzambia huyo.

Alisema kitu ambacho kilimuwia vigumu ni kucheza na wachezaji ambao anafanya nao mazoezi kila kukicha, Ibrahim Hamad 'Bacca' na Bakari Mwamnyeto katika mechi kati ya timu za Zambia na Tanzania.

"Haikuwa rahisi kucheza na wachezaji ambao mnafanya nao mazoezi kila siku, lakini kila mmoja alikuwa amesahau mambo ya klabu anapigania taifa lake," alisema.

Tanzania na Zambia zote zilikuwa kundi F, na ndizo zilizoaga mashindano, huku mechi yao ikiisha kwa sare ya bao 1-1.

Akizungumzia usajili wa wachezaji wapya kwenye kikosi cha timu yake na ushindani wa namba, alisisitiza kuwa ushindani upo kwenye klabu yoyote duniani.

"Ushindani ni mzuri na ushindani upo kwenye klabu yoyote duniani, najua wachezaji wengine wamesajiliwa kwa ajili ya kuja kuongeza nguvu ili timu ifanye vizuri, lazima kila mmoja apambane" alisema Musonda.

# Michezo

Jumamosi Januari 27, 2024

Nipashe


**Mbappe afikiria ofa ya Real Madrid na PSG** UKURASA 21





Samatta akimiliki mpira wakati wa mchezo wa fainali za Afcon dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo uliochezwa Jumatano iliyopita nchini Ivory Coast, timu hizo hazikufungana **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA, YANGA, AZAM ZAGEUKIA FA CUP

●●● Bodi ya Ligi yatangaza kuanza na michuano hiyo kabla ya michezo ya....

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi Tanzania imetangaza kuwa baada ya timu ya taifa ya Tanzania 'Taifa Stars' kuondolewa kwenye fainali za AFCON zinazoendelea nchini Ivory Coast, sasa wataendelea na mechi za viporo za kombe la Shirikisho (FA).

Kutokana na ratiba kuingiliana, klabu za Simba, Yanga na Azam FC zenyewe hazijacheza michezo yao ya michuano hiyo na sasa watalazimika kwanza kuicheza kabla ya kugeukia michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi hiyo, Almasi Kasongo akizungumza jana alisema kulikuwa na baadhi ya mechi za Kombe la FA ambazo hazikuchezwa kwa sababu mbalimbali, ikiwemo ushiriki wa klabu za Simba, Yanga na Azam kwenye michuano ya kimataifa na michezo yao ndiyo itakayoanza kupigwa kabla ya Ligi Kuu.

"Kimsingi tutatanguliwa na michezo ya Kombe la FA ambapo kuna baadhi ya timu hazikucheza katika ile kalenda ya mwanzo kutokana na majukumu mbalimbali, utakumbuka Simba, Yanga na Azam zilikuwa kwenye michuano ya kimataifa, kwa hiyo tutarudi na kuanza mechi za FA mbili tatu halafu baada ya hapo tutaendelea na mechi za Ligi Kuu pale tulipoishia," alisema Kasongo.

Aidha, alisema tarehe rasmi za michezo hiyo zitatangazwa hivi karibuni baada ya kukubaliana.

Ratiba ya Kombe la FA inaonyesha kuwa Yanga itacheza dhidi ya Haulung FC ya Njombe, Simba itakipiga na Tembo ya Kigoma, huku Azam ikitarajia kucheza dhidi ya Alliance FC ya Mwanza.

Kasongo alisema kutokana na Taifa Stars kutolewa, moja kwa moja kikanuni inaruhusu michuano ya ndani ikiwemo Ligi Kuu kuendelea kwa sababu hakuna tena timu yoyote ya Ligi Kuu iliyokuwa na wachezaji watatu kwenye timu ya taifa inayoshiriki AFCON.

"Kutokana na mataifa yenye idadi kubwa ya wachezaji wanaocheza klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara kutolewa kwenye fainali za AFCON zinazoendelea nchini Ivory Coast, kanuni za ligi zinatoa mwanya wa majadiliano ya tarehe za uendeshaji.

INAENDELEA UK. 23

# Musonda arejea kuipa Yanga ubingwa

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya timu ya taifa ya Zambia kutupwa nje ya fainali za Mataifa ya Afrika 'AFCON' yanayoendelea nchini Ivory Coast ikiwa kwenye hatua ya 16 bora, mshambuliaji wa timu hiyo, Kennedy Musonda amesema sasa ni wakati wa kurejea kwenye kikosi chake cha Yanga ili kuisaidia kutwaa Ubingwa wa Tanzania Bara.

Musonda ambaye alikuwa kwenye kikosi cha Zambia jana alirejea nchini kwao na sasa anajiandaa kurejea Tanzania haraka iwezekanavyo kuitumikia timu yake.

Nyota huyo alisema kuna mambo aliyoyapata kwenye michuano hiyo ambapo anaamini yatamsaidia katika kuitumikia timu yake hiyo ya Yanga.

"Hii ni mara yangu ya kwanza kucheza fainali za AFCON, hivyo kwangu ni historia, tumeshindwa lakini ndiyo mpira kwa sababu kila nchi ilikuwa inataka kufuzu, sasa narejea Dar es Salaam kwenye klabu yangu ya Yanga, kile kiwango nilichokionyesha kwenye mechi za kikosi changu cha taifa ndicho hicho nataka kukionyesha kwenye klabu yangu, na kuna vitu nimejifunza kwenye michuano hii ambavyo ni vya faida kwangu kama mchezaji na nitavitumia kwa ajili ya kuinufaisha klabu ya Yanga, nawaambia mashabiki nashukuru kwa sapoti yao, narejea ili tupambane tushinde mechi za Ligi Kuu," alisema Musonda.

Hata hivyo alisema hakupata shida sana kwenye michuano hiyo kwa sababu ametoka kwenye klabu kubwa iliyokuwa inacheza mechi za Ligi ya Mabingwa na wachezaji wakubwa.

"Yanga ni timu kubwa inayocheza Ligi ya Mabingwa, imenisaidia kwa sababu hata kiwango changu kwenye AFCON kimeongezeka, haikunipa tabu sana kwa sababu baadhi ya wachezaji tuliokuwa tunacheza

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042